

MAFUNDISHO YA PAULO

(MWALIMU)



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Kwanza

MAFUNDISHO YA PAULO
VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
(MWALIMU)

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Kwanza

Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study

J3 - 1Ts

Used by permission of International Publications Services

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, NAIROBI

© Copyright, 1986
Baptist Publications House
All rights reserved

YALIYOMO

SURA

UKURASA

1. Paulo Amtukuza Mungu	5
2. Wote Wamefanya Dhambi	10
3. Wote Wanaweza Kuokolewa	15
4. Ushindi Katika Kristo	21
5. Kukua Katika Kristo	26
6. Lengo La Maisha	32
7. Je! Nani Anayenimiliki	37
8. Uhuru Na Wajibu	42
9. Jamaa Ya Kikristo	46
10. Msaidizi Mkuu	51
11. Mungu Wa Rehema	55
12. Yesu Alikufa Kwa Ajili Yetu	59
13. Kristo Amefufuka	63

PAULO AMTUKUZA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Wagalatia 1:13-24

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Somo la wiki hii ndilo la kwanza kabisa katika masomo ya miezi mitatu hiyo yaitwayo "Mafundisho ya Paulo." Somo hili linalo ushuhuda wa Paulo jinsi alivyokutana na Kristo na jinsi maisha yake yalivyobadilishwa. Maisha yake yalibadilika kabisa. Alimtukuza Kristo alipotoa ushuhuda wake.

Utatakiwa kufanya mambo yafuatayo unapojitayarisha kwa ajili ya somo hili:

1. Omba kwa ajili ya uongozi unapojifunza na kujiandaa.
2. Soma kwa makini maandiko ya Biblia pamoja na kitabu hiki.
3. Soma somo hilo katika kitabu cha wanafunzi.
4. Uwe na mpango wa utaratibu jinsi utakavyofundisha ukweli wa somo hili.
5. Watembelee wanafunzi wako na wale wanaopaswa kuwa katika darasa lako.

Utatakiwa kusoma Matendo 9:1-22 ili uelewe vizuri somo hili. Hii ni hadithi inayoeleza jinsi Paulo alivyokutana na Yesu akiwa njiani akielekea Dameski. Paulo anazungumzia mambo matatu ambayo unapaswa kujua.

1. Maisha yake kabla ya kuokolewa: Alisema kuwa alikuwa Myahudi mwema. Aliwatesa Wakristo kwa sababu alifikiria kuwa walikuwa

wakifundisha uongo waliposema kwamba Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa.

2. Jinsi alivyokutana na Kristo: Alikuwa ameruhusiwa kwenda Dameski na kuwatesa Wakristo wa huko. Jambo hili lilitendeka alipokuwa njiani. Palitokezea ghafula nuru toka mbinguni na sauti ikasikika ikimwambia, "Sauli, Sauli, mbona waniudhi?" (Jina Paulo kwa Kiebrania ni Sauli. Soma Matendo 13:9). Yesu alimfahamu vizuri sana na akamwita kwa jina lake.

3. Itiko la Paulo: Paulo alianguka chini na akauliza, "U nani wewe, Bwana?" Alimtambua Yesu kuwa Bwana. Mwishowe Paulo alitii kwa kufanya yale aliyoambiwa na Kristo. Aliamini na akaokolewa.

Maandiko yetu ya leo ni Wagalatia 1:13-24. Paulo aliandika maneno haya katika barua na kuyatumia makanisa ya Galatia. Alikuwa amefika huko na kuwapelekea habari ya Injili wakati wa safari ya umisheni wake wa kwanza. Aliwaandikia jinsi Kristo alivyobadili maisha yake.

Paulo alikuwa mtu wa dini. Alikuwa Myahudi mwaminifu na mwalimu wa imani ya Kiyahudi. Alilitesa kanisa kwa sababu aliamini kwamba Mungu alinena kupita kwa Musa, wala si Yesu (Kifungu cha 13 na 14).

Mungu alimchagua na kumwita Paulo kuwa mtume. Tukio hili lililompata Paulo akielekea Dameski lilibadilisha maisha na nia yake.

Ulikuwa mwujiza wa neema ya Mungu. Mungu alimchagua Paulo kuwahubiria watu wa Mataifa. Alikuwa mwaminifu kwa mwito wake na akawa mmisheni wa kwanza katika Agano Jipya.

Waamini walimtukuza Mungu kwa ajili ya ushindi wa Paulo. Mwanzoni hawakuamini kuwa Paulo alikuwa akisema ukweli. Wakristo walimjua kama mtesaji wa kanisa. Walimwogopa na wakaanza kumwuliza maswali. Paulo alijidhihirisha mwenyewe kwa yale aliyosema na jinsi alivyoishi. Hatimaye Wakristo walimwamini. Wakamtukuza Mungu kwa ajili ya maisha mapya ya Paulo.

Paulo alimtukuza Kristo. "Kumtukuza inamaanisha "ku-heshimu". Paulo aliwaheshimu watu wengine, kama mwalimu wa Kiyahudi. Hata hivyo, yale aliyofanya hayakumtukuza Kristo. Yeye angekuwa tu mwalimu wa Kiyahudi ikiwa angetaka kujitukuza mwenyewe. Lakini alipookolewa alitaka kumtukuza Kristo kuliko mtu mwingine ye yote. Alimtukuza Kristo katika njia hizi mbili:

1. Kama shahidi wa Kristo. Kuna mahali patatu katika Agano Jipya ambapo panaeleza kuongoka kwa Paulo. Yeye mwenyewe alisimulia hadithi hii mara nyingi.

2. Kama Mhubiri. Paulo alitembelea sehemu mbalimbali akiwa na ujumbe wa Injili. Aliwahubiria Wayahudi, na Watu wa Mataifa, wafalme na hata gerezani. Hakuionea haya Injili. Aliwataka watu wengi wamjue Kristo na wamfuate.

Wawezaje kumtukuza Kristo? Ukiwa mwalimu waweza kumtukuza kwa kuwasaidia wanafunzi kumjua Kristo na kumfuata. Hivi ndivyo Paulo alivyomtukuza Kristo. Kwanza, utahitaji kuimarisha uhusiano wako na Kristo. Wewe ni kama mfano kwa wale unaofundisha. Wanapaswa kuona jinsi Kristo alivyobadili maisha yako jinsi unavyoishi.

Kusudi la Somo Hili ni kuwasaidia wanafunzi ambao hawajaokolewa kuweza kufahamu jinsi ya kumpokea Kristo kama Mwokozi wao. Kuwasaidia waamini ili waweze kujifunza jinsi wawezavyo kumtukuza Kristo katika maisha yao.

KUFUNDISHA SOMO

Sema: Hebu fikirieni kuhusu mvulana au msichana ambaye ni mbaya sana katika shule yako.

Uliza: Je, ungefikiriaje kama ungesikia kwamba amemwamini Kristo? (Wape muda wa kujibu). Andika jina PAULO ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Sema: Paulo alikuwa jinsi hiyo. Alikuwa mwenye dhambi.

Uliza: Ni yapi ujuayo kuhusu Paulo? (Andika majibu yao ubaoni.) (Waweza kusema: aliwatesa Wakristo, aliwaruhusu watu wamwue Stefano, hakuwapenda wafuasi wa Yesu, alikuwa mmisheni na aliandika vitabu vingi vya Agano Jipya.)

Eleza kuhusu maisha ya Paulo na jinsi alivyobadilishwa. Tumia maelekezo yaliyosemwa katika kitabu cha wanafunzi. Baadhi ya hayo ni:

1. Alizaliwa Tarso.


2. Alikuwa Myahudi, na pia raia wa Rumi.
3. Alikuwa mwenye kisomo. Kwanza alisomea nyumbani kwao, halafu akaenda Yerusalemu kujiendeleza.
4. Alifundishwa na Gamalieli alipoenda Yerusalemu.
5. Alikuwa mwalimu wa Wayahudi.

Uliza: Wayahudi waliaminije kuhusu Yesu? (Waliamini kwamba Yesu alikuwa mwalimu wala sio Masihi aliyeahidiwa.)

Sema: Paulo aliamini kwamba Wakristo walipaswa kuadhibiwa kwa kufundisha uongo kuhusu Yesu. Yeye alifikiria kuwa alikuwa akimpendeza Mungu kwa kuilinda imani ya Wayahudi.

Uliza: Paulo aliokolewaje? (Ngojea majibu.) Endelea kueleza hadithi ya kuongoka kwa Paulo ukitumia madokezo yafuatayo:

1. Paulo na wenzake walikuwa wakienda Dameski ili kuwatesa Wakristo wa huko.
2. Walipokuwa njiani waliangaliwa na nuru kuu kutoka mbinguni.



3. Sauti ilisikika ikimwambia, "Sauli, Sauli, mbona waniudhi?"
4. Paulo alifanywa kipofu.
5. Yesu alimwambia kwenda katika mji ule na kungoja hadi atakapomwambia jambo la kufanya.
6. Mungu alimtuma Anania kwake. Alimsaidia Paulo naye akaweza kuona tena.
7. Paulo aliweza kubadilishwa kabisa.

Soma maandiko ya Biblia. Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wagalatia 1:15.

Uliza: Je, Mungu alimwagiza Paulo afanye kazi gani? (Kuwahubiria watu wa mataifa Habari Njema.)

Uliza: Paulo alimtukuzaje Kristo? (Alieleza jinsi Kristo alivyobadili maisha yake na akawahubiria watu wengine Habari Njema.)



Mwambie mwanafunzi mwingine asome Wagalatia 1:21-24.

Uliza: Wakristo waliitikiaje mahubiri ya Paulo? (Mwanzoni hawakumwamini, lakini baadaye walianza kumshukuru Mungu kwa ajili yake.)

Uliza: Wawezaje kumtukuza Kristo? (Kwa kushuhudia jinsi Kristo

alivyoyabadilisha maisha yako, na kuwaambia wengine habari zake.)

Rudia tena ushuhuda wa Paulo.

1. Eleza vile alivyokuwa kabla ya kuokolewa.
2. Eleza jinsi alivyokutana na Yesu.
3. Eleza jinsi maisha yake yalivyobadilishwa baada ya kuokolewa.

Tumia mtindo huo huo na uwasaidie wanafunzi kujua jinsi wawezavyo kuwatolea watu wengine ushuhuda wao. Wahimiza ili waweze kumweleza mtu mmoja wiki hii jinsi walivyo mwamini Yesu kama Mwokozi wao.

KAZI YA KUFANYA

Je, Yesu anaishi ndani yako sasa? Andika jina lako katika nafasi hii ikiwa anaishi moyoni mwako. (Jina la mwanafunzi) _____

Kama Yesu haishi moyoni mwako, angependa kuanza sasa. Anataka awe Bwana na Mwokozi wako. Anakutaka umtukuze jinsi Paulo alivyofanya.

Jibu Maswali yafuatayo:

1. Paulo alikuwa akienda mji upi alipoangaziwa na nuru kutoka mbinguni? DAMESKI
2. Je ni nani aliyenena na Paulo? YESU
3. Macho ya Paulo yalifanyaje? YALIPOFUKA

Tumia maneno haya kwa kukamilisha hadithi ifuatayo:

Myahudi	Gamalieli
Yerusalemu	Yesu
Rumi	Tarso
Stefano	Dameski

Alikuwa pia raia wa RUMI. Alipokuwa yungali kijana alienda kusomea YERUSALEMU akifundishwa na mwalimu aitwaye GAMELIELI. Paulo alikuwa mtu wa dini sana, lakini hakumwamini Yesu. Aliwatesa wafuasi wa Yesu. Siku moja alimwona STEFANO akiuawa kwa kupigwa mawe. Yesu alinena naye alipokuwa njiani akielekea DAMESKI. Baadaye aliamini na akawa mfuasi wa YESU.

Wape muda wa kuandika ushuhuda wa Paulo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Wakamtukuza Mungu kwa ajili yangu" (Wagalatia 1:24).

Andika kifungu hiki ubaoni. Futa neno moja moja baada ya kusemwa.

Waambie waseme maneno ya "kutukuza". (Ya kumsifu Mungu.)

Wape muda wa kuweza kuandika njia ambazo watamtukuza Mungu kwazo wiki hii.

Ombeni pamoja. Mwombe Mungu amsaidie kila mwanafunzi ili amtukuze Kristo jinsi alivyoandika. Mwombe ye yote ambaye hajaokoka na anahitaji kumwamini Kristo kama Mwokozi wake.

Tumia mfano wa mviringo uliochora ubaoni kwa kufanyia zoezi hili. Tumia kifaa kidogo kama raba ya kufutia, au mpira mdogo au kishale. Mwambie mwanafunzi mmoja ajaribu kulenga katikati.

Sema: Mungu anatumia tuwe watakatifu. Lakini hatuwezi kujitakasa kwa sababu ya hali yetu ya dhambi.

Huwa tunakosa shabaha kila mara,
kwa sababu ya dhambi tulizonazo.

Mwambie mwanafunzi mmoja
asome Isaya 59:1-2.

Sema: Dhambi zetu hututenganisha
na Mungu lakini Kristo hurudisha
uhusiano huo katika kifo chake.
Tunapomwamini, yeye huzichukua
dhambi zetu na kututenganisha nazo
kabisa.

WAKATI WA MWISHO

Uliza kama kuna ye yote ambaye
angetaka kumwamini Yesu kama
Mwokozi, wake. Mwambie ye yote
ambaye angependa kujua mengi
kuhusu wokovu abaki nyuma wengine
waondokapo.

Ombeni pamoja. Mshukuru Mungu
kwa ajili ya upendo wake mkuu wa
kumtuma Mwanawe kufia dhambi
zetu. Mwombe awasaidie wale
wanaotaka kumwamini Yesu kama
Mwokozi wao kuwa na moyo wa
kufanya hivyo leo.

Imba pamoja, "Mungu Yu Mwema".

WOTE WAMEFANYA DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Warumi 1:18-25

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Biblia ni hadithi ielezayo dhambi za mwanadamu na wokovu wa Mungu. Mwanadamu alitenganishwa na Mungu alipofanya dhambi. Hangeweza kushirikiana naye jinsi ilivyokuwa hapo awali. Mwanadamu alifukuzwa kutoka katika Bustani ambayo Mungu alikuwa amempandia. Hangeweza tena kufurahia uzuri wa yote ambayo Mungu alikuwa amemwambia.

Somo letu la leo lahusu ukweli huu: Dhambi ya mwanadamu na wokovu wa Mungu katika Kristo.

Utatakiwa kufanya yafuatayo unapötayarisha somo hili:

1. Omba kwa ajili ya uongozi unapöjifunza na kujiandaa.
2. Soma Maandiko ya Biblia ukitumia kitabu hiki pamoja na kile cha mwanafunzi.
3. Uwe na mpango wa utaratibu jinsi utakavyo fundisha somo hili.
4. Hebu yafikirie maisha yako. Je, una dhambi ambayo ungependa kutubu? Je, wewe ni mfano mwema kwa wanafunzi wako kama mwalimu?
5. Hebu wafikirie washiriki wako. Je, unawafahamu wale waliomwamini Yesu kama Mwokozi wao? Je, unajua wale ambao hawajaokoka.
6. Andika mambo yote ujuayo juu ya kila mwanafunzi katika kitabu. Andika jina moja katika kila ukurasa. Andika

anwani yake, majina ya wazazi wake, matatizo yake yote unayofahamu na mambo unayotaka kumwombea.

Soma Warumi 1:18-20. Hapo mwanzo mwanadamu alimfahamu Mungu. Mungu alijidhihirisha kwa mwanadamu kupitia kwa muumbo wake. Mwanadamu angeangalia kila sehemu na kujua kwamba kuna Mungu aliyeumba mbingu, ardhi, wanyama, ndege, miti naye mwenyewe. Hangeweza kusema kwamba hakukuwa na Mungu.

Soma Warumi 1:21-23. Mwanadamu alimkataa Mungu alipotenda dhambi. Alichagua kuusikiliza uongo wa Shetani badala ya kuusikiliza ukweli wa Mungu. Alianza kuabudu miungu alioitengeneza mwenyewe badala ya kumwabudu Mungu wa kweli. Mwanadamu alitaka kutumia muumbo wa Mungu, lakini hakutaka kumshukuru wala kumsifu Mungu kwa ajili yavyo.

Soma Warumi 1:24-26. "Mungu aliwaacha" kwa ajili ya dhambi zao. Tunasoma mara tatu kwamba "Mungu aliwaacha." Mungu alikuwa yungali anampenda mwanadamu kama hapo mwanzo, lakini mwanadamu naye akaharibu ushirika wake na Mungu. Akachagua kutomtii.

Mwanadamu hakutubu alipotambua matokeo ya dhambi zake. Badala yake aliendelea kuwa mbaya sana. Kifungu cha 25 kinaeleza matendo yake:

1. Aliufanya ukweli wa Mungu kuwa uongo, na

2. Alisujudia na kuabudu viumbe badala ya muumba wake. Alitenda dhambi kiwazi na akawahimiza wenzake kumfuata katika kutenda dhambi.

Vifungu hivi vinatufanya tujihoji mioyoni mwetu. Je, tunatumiaje marifa tuliopewa na Mungu? Wale ambao hawamjui wamepotea na wanahitaji kuokolewa. Tunajua dawa ya ugonjwa wao. Sisi kama Wakristo tunalo jukumu la kuishi maisha ya Kikristo, na kuwaambia jinsi ya kuokolewa.

Kusudi la somo hili ni *kuwasaidia wanafunzi kujua jinsi ya kupatana na Mungu kwa kumwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wao.*

KULIFUNDISHA SOMO

Wasimulie hadithi ifuatayo katika maneno yako mwenyewe:

Yakobo alikuwa kijana aliyeishi katika mji mmoja mkubwa. Kulikuwa na shida nyumbani kwao kwa hivyo alikuwa akienda huko kula tu na kulala. Alikuwa akiendelea vizuri na masomo yake hadi darasa la sita. Lakini, hatimaye alianza kupatwa na shida. Angewadanganya wazazi wake kuwa anaenda shuleni, kumbe hakuwa akihudhuria masomo. Hivyo alianza kukosa kufanya vizuri masomoni. Mwishowe aliacha shule kwa sababu ya kuanguka mtihamu na kutohudhuria.

Yakobo alikuwa na muda mwingi alipoacha shule. Kulikuwa na vijana wengine pale kijijini nao hawakuwa wakisoma. Walianza kukusanyika na kutembea pamoja. Marafiki hao wa Yakobo hawakuwa wenye tabia nzuri. Mmoja wao alianza kuiba sigara za

babake na kuzileta ili wavute pamoja. Baadaye, mwingine aliiba pesa ili waende kunywa pombe. Kila tendo moja baya lilianzisha lingine. Muda si muda, polisi waliwapata wakivunja ghala ya wenyewe. Walishikwa na kupelekwa katika kituo cha polisi. Walipohojiwa walipatwa na hatia na wakaadhibiwa kwa kukosa kwao.

Shida ya Yakobo ilianza kwa kuwadanganya wazazi wake. Jambo hili lilimfanya aanze kuanguka mtihamu, halafu kuacha shule, na kuchagua kundi la marafiki wabaya, kuanza kuiba na mwishowe kuadhibiwa kwa kutenda makosa. Kosa moja lilianzisha lingine.

Uliza: Nataka mfikirie njia ambazo Yakobo angetumia ili asipatwe na shida. (Wape muda wa kujibu.)

Andika neno DHAMBI ubaoni au kwenye karatasi kubwa.

Uliza: Je, maana ya "dhambi" ni nini? Pengine baadhi yao watakumbuka yale tuliyojifunza wiki iliyopita kuhusu dhambi. (Andika majibu yao ubaoni. Majibu hayo yanapaswa kuwa hivi: dhambi ni kutomtii Mungu, kufanya yale utakayo badala ya yale Mungu atakayo, kufuata njia yako mwenyewe badala ya ile ya Mungu, kukosa lengo au shabaha.)

Mwulize mshiriki mmoja kusoma Warumi 3:23.

Uliza: Nataka mtaje dhambi ambayo hutendwa na vijana. (Kudanganya, kusema uongo, kulitaja bure jina la Mungu, kutowatii wazazi, kutamani, kuwa na hasira, kujivuna, kufanya mapenzi nje ya ndoa, kusengenyana, kutumia madawa ya kulevya)

Uliza: Mungu husikiaje tutendapo dhambi? (Ngojea majibu. Mungu hapendi dhambi lakini hapendi dhambi mwenye dhambi.)

Mwambie mshiriki mwingine asome Warumi 1:18.

Uliza: Mungu alifanyaje ili kudhihirisha kwamba alimpenda mwenye dhambi lakini hapendi dhambi zake? (Alimtuma Mwanawe kufia dhambi zetu ili sisi nasi tusiadhibiwe.)

Mwambie mshiriki mmoja asome Warumi 1:19-24.

Uliza: Je, mwanadamu ana kisingizio gani kwa kutokumwamini Mungu? (Hana kisingizio cho chote.)

Paulo alikuwa akiwaandikia watu wa Mataifa waliokuwa wakiabudu miungu. Walimjua Mungu kupitia kwa muumbo wake. Wayahudi hawakuwa na kisingizio kwa sababu Mungu alikuwa amejidhihirisha kwao tokea enzi za Ibrahimu. Watu wa siku hizi nao hawana kisingizio.

Uliza: Je, matokeo ya dhambi ni nini? Je, ikiwa mtu atanza kusema uongo, matokeo yake yatakuaje? (Taja mambo kama kula madawa ya kulevya, usherati, kusengenyana, na kuiba.

Chora mfano wa duara (mviringo) ubaoni na uweke kiduara kidogo katikati (nukta). Waweza kuja na ubao wa mchezo wa kurusha mshale kama uko nao.

Sema: Paulo alieleza maana ya Warumi 3:23 kwa kutumia mfano wa mtu aliyelenga shabaha kwa kutumia uta na mshale. Maisha matakatifu ya Kristo yanapaswa kuwa lengo au shabaha ya kila mwamini. Dhambi



tutendayo hutufanya tukose shabaha, au lengo ambalo Mungu ametuwekea.

Mungu ni mtakatifu na hawezi kuvumilia dhambi. Dhambi zetu hututenganisha na Mungu na hutufanya tusiweze kushirikiana naye.

Lakini Mungu anatupenda hata ingawa tu wenye dhambi.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Warumi 5:8.

Sema: Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa wenye dhambi. Upendo wa Kristo kwetu ulimfanya kulipa deni la makosa yetu.

Uliza: Je, tunahusianaje na Mungu baada ya kumwamini Yesu na kusamehewa dhambi zetu? (Hupatanishwa, na kufanywa wenye haki, na kuurudia tena uhusiano wetu na Mungu.)

Mwambie mwanafunzi mwingine asome Yohana 1:12.

Uliza: Je, inamaanisha nini kuwa mtoto? (Tuna jamaa, na tuna haki ya kushiriki katika vyote ambavyo baba anavyo.)

Uliza: Je, mtu anapaswa kufanyanje awe mwana wa Mungu? Eleza jinsi ya kuokolewa:

1. Tubu: Kutubu inamaanisha kwamba ufahamu kuwa wewe u mwenye dhambi, na sasa uache dhambi zako na uanze kumwamini Yesu.

2. Kukiri: Maana ya kukiri ni kukubaliana na Mungu kuwa umetenda dhambi. Taja maovu uliyomtendea Mungu. Mwambie jinsi ulivyokosa kumtii.

3. Amini: Yesu alilipa deni la dhambi zetu alipokufa msalabani. Lazima tuamini kuwa ametusamehe dhambi zetu zote.

4. Mwamini Yesu: Kumwamini Yesu ni kukubali msamaha wa Mungu wa dhambi zetu na kumruhusu Kristo kuwa Bwana wa maisha yetu.

KAZI YA KUFANYA

Chora msitari hadi kwa maneno yanayokamilisha vyema sentensi ifuatayo.

Paulo aliandika hakuna amefanya dhambi.
kwamba

wachache wamefanya dhambi.

wote wamefanya dhambi.

Weka alama (✓) katika kisanduku cha sentensi iliyosahihi.

____ Paulo alikuwa akitembelea mji wa Rumi kabla ya kuwaandikia barua Wakristo wa huko.

✓ ____ Paulo hakuwa amefika Rumi alipowaandikia Warumi barua hii.

____ Warumi 3:23 inasema kwamba watu wengi wametenda dhambi.

✓ ____ Kutenda dhambi ni kukosa shabaha.

✓ ____ Kutomtii Mungu ni kutenda dhambi.

____ Dhambi hututenganisha na Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23).

Tumia mfano wa mviringo uliochora ubaoni kwa kufanyia zoezi hili. Tumia kifaa kidogo kama raba ya kufutia, au mpira mdogo au kishale. Mwambie mwanafunzi mmoja ajaribu kulenga katikati.

Sema: Mungu anatutaka tuwe watakatifu. Lakini hatuwezi kujitakasa kwa sababu ya hali yetu ya dhambi. Huwa tunakosa shabaha kila mara, kwa sababu ya dhambi tulizonazo.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Isaya 59:1-2.

Sema: Dhambi zetu hututenganisha na Mungu lakini Kristo hurudisha uhusiano huo katika kifo chake.

Tunapomwamini, yeye huzichukua dhambi zetu na kututenganisha nazo kabisa.

WAKATI WA MWISHO

Uliza kama kuna ye yote ambaye angetaka kumwamini Yesu kama Mwokozi, wake. Mwambie ye yote ambaye angependa kujua mengi kuhusu wokovu abaki nyuma wengine waondokapo.

Ombeni pamoja. Mshukuru Mungu kwa ajili ya upendo wake mkuu wa kumtuma Mwanawe kufia dhambi zetu. Mwombe awasaidie wle wanaotaka kumwamini Yesu kama Mwokozi wao kuwa na moyo wa kufanya hivyo leo.

Imba pamoja, "Mungu Yu Mwema".

WOTE WANAZEWA KUOKOLEWA

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 3:16;
1 Timotheo 2:3-7

KUJIANDAA KUFUNDISHA

"Wote wanaweza kuokolewa," haya ni baadhi ya maandiko ya ukweli yaliyoandikwa na Paulo. Kulikuwa na wakati ambapo Paulo aliamini kwamba Wayahudi tu ndio wangemjua Mungu na kupewa wokovu wake. Aliamini kwamba Wayahudi walikuwa wateule wa Mungu na watu wengine hawakustahili upendo wala neema ya Mungu.

Maisha ya Paulo yalibadilika alipokutana na Yesu. Alikuwa Myahudi, lakini Mungu alimtumia kwa watu wa Mataifa kama mmisheni. Mungu alinena na Anania, Mkristo aishiye Dameski wakati Paulo alipokutana na Yesu. Akamwambia, "Nenda tu, kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukua jina langu mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli" (Matendo 9:15). Anania alienda na akamwekea Paulo mikono. Aliweza sasa kuona kimwili na kiroho. Paulo alianza sasa kuwaambia watu habari za upendo wa Mungu ulioko katika Yesu. Aliamini kwamba Yesu alifia dhambi zake naye aliwataka wengine nao waamini na kuweza kumpokea.

Utatakiwa kufanya yafuatayo unapotayarisha somo hili:

1. Mwombe Mungu akusaidie unapofundisha somo hili.
2. Soma maandiko ya Biblia. Anza kuyasoma mapema. Usingoje ifikapo

Jumamosi ndipo uanze kujifunza somo lako. Mungu atatumia yote yaliyotendeka kwako wakati wa wiki ili kuwawezesha watoto kuelewa yale uwafundishayo.

3. Hebu wafikirie washiriki wa darasa lako. Je, kuna wale wanaotaka kumwamini Kristo kama Mwokozi wao? Unapofundisha somo hili wasaidie kuelewa maana ya "kuzaliwa mara ya pili". Utatakiwa kueleza kwamba "kuzaliwa mara ya pili" na "kuokolewa" yote haya yana maana moja.

4. Fanya orodha ya mpango wa kufundisha.

a). Linganisha somo hili na lile la wiki jana, "Wote Wamefanya Dhambi."

b). Rudia sehemu ya hatua za jinsi ya kuokolewa.

5. Chagua watu wawili wawezao kusoma vizuri kuchukua mahali pa Yesu na Nikodemo katika mchezo huu. Soma sehemu ya mchezo huo pamoja nao kabla ya kuanza darasa ili waweze kushiriki vyema.

6. Waombe wanafunzi wako. Mwombe Roho Mtakatifu kumwongoza ye yote ambaye angependa kuokolewa ili amwamini Kristo wiki hii. Usiwalazimishe wanafunzi wako kufanya uamuzi wao. Mwachie Roho Mtakatifu amwongoze kwa kufanya hivyo.

Soma Yohana 3:1-16. Nikodemo alikuwa mmoja kati ya wakuu wa

Wayahudi ambao lengo lao lilikuwa kulinda sheria za dini ya Kiyahudi. Washiriki wa kamati hii walijulikana kama Mafarisayo. Mafarisayo walionekana kuwa watu walioshika dini sana, lakini Yesu aliifahamu mioyo na mawazo yao. Aliwaita wanafiki, wapumbavu, nyoka na viongozi vipofu. (Mathayo 23)

Kulikuwa na Mafarisayo wengine ambao walimwamini Yesu kwa siri. Nikodemo alikuwa mmoja wao ambaye alitaka kufahamu Yesu vizuri. Akamwendea wakati wa usiku. Biblia haitwambii hasa sababu yake ya kumwendea Yesu usiku. Pengine huo ndio wakati ambao angeweza kumwona Yesu akiwa peke yake. Au, huenda hakutaka Mafarisayo wengine kujua kuwa amemwendea Yesu. Hata hivyo, Nikodemo alitaka kufahamu zaidi habazi za Yesu na mafundisho yake.

Nikodemo alimtambua Yesu kama "mwalimu aliyetoka kwa Mungu." Alisema kwamba hakukuwa na awezaye kufanya yale ambayo Yesu alifanya kama hakuwa pamoja na Mungu. Yesu alimjibu kwa kusema kuwa - "Amini, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3).

Nikodemo akauliza, "Awezaje mtu kuzaliwa tena akiwa mzee? Yesu hakumaanisha hivyo. Alikuwa akisema kuhusu kuzaliwa kiroho wala sio kimwili. Lilikuwa jambo ambalo halingeweza kuonekana, lakini yangukuwa mabadiliko katika maisha ya mtu aliyeamini.

Yesu alitumia mfano wa upepo kwa kuelezea mafundisho yake. Si rahisi kuuona upepo. Hali matokeo yake yaweza kuonekana. Hakuna ajuaye mahali upepo utokapo wala uendapo. Hali anajua kwamba upepo upo.

Uzao mpya ni jambo la Kiroho. Mtu hawezi kubadilika kwa sura au maumbile. Lakini, aliyeamini anafahamu kwamba maisha yake yamebadilika. Huwa amezaliwa upya nalo ni tendo kama upepo uvumao.

Yesu alisema kwamba uzao huu mpya ni kwa maji na roho. Nikodemo alikuwa mwanafunzi wa Agano la Kale. Ingekuwa rahisi kwake kujua kwamba Yesu alikuwa akitumia vifungu vya Ezekieli 36:25-27. Mungu akawaambia, "Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi...Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu."

Yesu alimkumbusha Nikodemo tukio lililowapata Waebrania walipokuwa jangwani. Waliadhibiwa na nyoka kwa sababu ya dhambi zao. Mungu alimwagiza Musa kutengeneza nyoka wa shaba na kumwinua juu pale kambini. Mtu angeweza kuponywa baada ya kuumwa alipomwangukia nyoka yule aliyeinuliwa.

Yesu alikuwa akimwambia Nikodemu kwamba watu wanapaswa kumwangukia ili waponywe dhambi zao. Hasa wanapaswa kuuangukia msalaba ili waokoke jinsi Waebrania walivyo mwangukia nyoka wa shaba na wakaokoka.

Katika mwisho wa kitabu cha Yohana tunasoma kwamba Nikodemo alikuwepo wakati wa kusulubiwa kwa

Yesu. Yeye pamoja na Mfarisayo mwingine aitwaye, Yusufu wa Arimatheya, waliutayarisha mwili wa Yesu na kwenda kuuzika. Nikodemo alinunua manukato ya bei ghali sana na kuupaka mwili wa Yesu wakati wa mazishi. Inaaminika kwamba alifuata yale aliyoambiwa na Yesu na akawa mwamini.

Soma 1 Timotheo 2:3-7.

Yesu alikuwa amemwambia Nikodemo kwamba wote ambao wangemwamini wangepata uzima wa milele. Baada ya kupita, Paulo naye alimwandikia Timotheo ujumbe huo huo alipokuwa akianza huduma yake kama mhubiri. Akamwambia, "Mungu... hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli" (1 Timotheo 2:4). Paulo aliendelea kueleza kwamba Yesu alitoa maisha yake kwa ajili ya jambo hili.

Nikodemo, na viongozi wengine wa kidini waliomsikiliza Yesu, waliamini kwamba wokovu ni kwa Wayahudi peke yao. Watu wa Mataifa hawakuwa katika mpango wa Mungu. Wayahudi ndio waliokuwa wateule wa Mungu ambao wangeokolewa naye. Hata hivyo, mpango wa Mungu tangu mwanzo ulihusu wokovu kwa watu WOTE. Alimtumia Paulo, Myahudi, kuupelekea ujumbe huu watu wa Mataifa. Mungu anampenda kila mmoja na Kristo alikufa ili awaokoe watu wote.

KULIFUNDISHA SOMO

Kusudi la somo hili ni *kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwamba wale wote wamwaminio Kristo kama Mwokozi wataokoka.*

Waambie wanafunzi hao waseme majina ya nchi za Afrika zilizopata uhuru. (Wasaidie ili wataje nchi nyingi wawezaavyo.)

Uliza: Je, ni nani wafaidikao na matokeo ya uhuru? (Watu wote)

Uliza: Je, watu watasikiaje ikiwa kabila moja litasema, 'Uhuru ni kwa ajili ya kabila letu'? (Makabila mengine hayatapendezwa na hivyo kutatokea matatizo au mizozo.)

Sema: Somo letu la leo linatufundisha kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote. Alizaliwa katika nyumba ya Kiyahudi, lakini aliwaletea watu wote wokovu, wala sio Wayahudi tu.

Watu wote hawakuamini kwamba hii ni kweli. Nikodemo alikuwa Myahudi na akiongozi wa kidini wa Wayahudi. Alijua sana sheria na alikuwa mmoja wa wakuu wa Kiyahudi waliohakikisha kwamba sheria inafuatwa. Nikodemo alikuwa na maswali, kwa hivyo aliamua kumwendea Yesu ili amjibu.

Waambie wale wanafunzi wawili uliochagua kuufanya mchezo wa Nikodemo na Yesu.

Uliza: Je, mnafikiri ni kwa nini Nikodemo alimwendea Yesu usiku? (Ngojea majibu. Biblia haelezi jambo hili. Pengine alitaka kuwa na Yesu peke yake, au hakutaka kuonwa na Mafarisayo wengine.)

Uliza: Je, Nikodemo alifanya nini kinachotufanya kuelewa kwamba alimjua na kumheshimu Yesu? (Alimwita Yesu, "Rabbi, au Mwalimu". Aliyaelewa pia mafundisho ya Yesu.)

Uliza: Je, Yesu alisema Nikodemo alipaswa kufanyaje? (Kuzaliwa mara ya pili?)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 3:3-11.

Uliza: Je, Yesu alitumia mfano upi kwa kueleza "kuzaliwa mara ya pili"? (Upepo)


Sema: Mtu azaliwapo mara ya kwanza huwa amezaliwa kimwili. Azaliwapo upya katika ufalme wa Mungu huwa amezaliwa Kiroho. Mtu hawi Mkristo kwa kuwa amezaliwa katika jamaa ya Kikristo. Ni lazima kila mmoja aamini na amkubali Kristo.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 3:14-16.

Uliza: Kwa nini Yesu alitumia mfano wa nyoka aliyewekwa juu ya mti kule jangwani? (Kama wanafunzi wako hawajawahi kusikia jambo hili, basi mwambie mmoja wao asome Hesabu 21:5-9.)

Sema: Watu wale wa jangwani walikuwa wamefanya dhambi. Mungu aliwaadhibu kwa kuwaletsa nyoka wa moto ili wauawe. Baadhi yao walikufa walipoumwa na nyoka hao. Mwishowe walimwendea Musa na kutubu dhambi waliyoitenda. Mungu alimwagiza Musa kujifanyia nyoka ya shaba na kumweka juu ya mti ili kila mmoja aweze kumwona. Wakati watu hao walipoumwa na nyoka wale walipaswa

kumwangukia yule aliyoko mtini na kuepuka kifo.




Uliza: Je, Yesu alikuwa akifundisha ukweli upi katika mfano huo? (Angekufa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Kifo chake msalabani kingekuwa hasa ndiyo njia ya watu kuweza kuponywa ugonjwa wao wa dhambi. Wangeokoka kama wangetubu dhambi zao na kumwamini Kristo.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome 1 Timotheo 2:3-7.

Sema: Mungu alimpa Paulo jukumu la kuwaambia Watu wa Mataifa ujumbe wa Injili. Yesu aliwapenda watu wote na akataka waokolewe. Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi za kila mmoja. Wayahudi na Watu wa Mataifa, matajiri na maskini, waliosoma na wasio na kisomo. Wote wangeokolewa.

Chora picha hii ubaoni au kwenye karatasi kubwa.



Sema: Mwanadamu alitenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Lakini Kristo alikufa msalabani ili kumpatanisha Mwanadamu na Mungu. Mungu aliiponya dhambi kwa kifo cha Mwanawe.

Uliza: Je, dhambi zako hukutenganisha na Mungu? Kwa nini usimwangelie Yesu pale msalabani na akuponye dhambi zako?

Waambie washiriki wako kufungua sehemu ya maombi katika somo lao. Someni sehemu hiyo pamoja.

Sema: Ikiwa unataka kumwamini Yesu leo kama Mwokozi wako, tafadhali baki nyuma baada ya somo hili na tutaongea pamoja.

Waambie wote waangalie katika "Hati ya kuzaliwa kiroho". Wahimiza wale ambao wameisha mwamini Yesu kama Mwokozi wao wajaze hati hiyo tarehe walipozaliwa kimwili na tarehe walipozaliwa kiroho.

KAZI YA KUFANYA

Waambie washiriki waandike jinsi ambavyo wanafikiria wamebadilika tangu walipomwamini Kristo. Wale ambao hawajaokoka hawapaswi kuandika cho chote kwani hawajatendewa lo lote na Kristo maishani mwao.

Waambie wanafunzi hao kuweka alama ya (✓) kwa swali hili, "Kwa nini niwe Mkristo?"

- ✓ Mungu anakupenda na anataka uokolewe.
- Wewe ni Mkristo kama jamaa yako ni Wakristo.
- ✓ Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako. Alilipa deni lako ili uwe na uzima wa milele.
- Unapaswa kufanya hivyo kwa sababu rafiki zako wote wameokoka.
- Waweza kushiriki katika meza ya Bwana ikiwa wewe ni Mkristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

Waambie washiriki hao waandike kwa herufi kubwa maana ya kusema Mungu anawapenda.

WAKATI WA MWISHO

Andika maneno yafuatayo ubaoni:

MUNGU	Mtoaji mkuu
ALIUPENDA	Ukweli mkuu
ULIMWENGU	Karama kuu
AKAMTOA	Nafasi kuu
MWANAWA	Ahadi kuu
YE YOTE AMWAMINIYE	Milki kuu
HATAPOTEA	
AWE NA UZIMA WA MILELE	

Gawa darasa hilo katika makundi mawili. Kundi moja litasoma maneno ya mkono wa kushoto na lingine yale ya mkono wa kulia. Semeni pamoja kifungu hicho, halafu umruhusu ye yote atakaye kukisema.

Ombeni pamoja. Mshukuru Mungu kwa ajili ya karama yake kuu ya kumtuma Yesu kama Mwokozi wa ulimwengu wote.

USHINDI KATIKA KRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Warumi 8:1-4, 35-39; Wagalatia 2:19-20

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wanafunzi walijifunza katika masomo yaliyopita kuhusu ukweli huu:

1. Ushuhuda wa Paulo jinsi alivyookolewa.
2. Wote wamefanya dhambi na wanahitaji msamaha wa Kristo.
3. Mungu aliwapenda watu wote na amelea njia ya wokovu katika Kristo.

Somo la leo linatia mkazo kwamba Kristo alishinda dhambi katika kufa, kuzikwa na kufufuka kwake. Shetani ameshindwa. Kwa hivyo, waamini wanaishi katika ushindi kwa sababu wako katika Kristo na Kristo yu ndani mwao. Tuko huru kutoka kwa hukumu ya Mungu, uwezo wa dhambi na kifo na woga wote. Ni haki na waajibu wetu kuishi katika ushindi. Kristo ndiye ushindi wetu.

Fikiria kuhusu yafuatayo unapotayarisha somo hili:

1. Je, wewe mwenyewe unaishi maisha ya ushindi? Unahitajika uifie nafsi yako na matakwa na kufanya Kristo awe Bwana wa maisha yako. Utatakiwa utii Neno lake na mafundisho yake.
2. Wafikirie wanafunzi wako. Je, wao ni waamini? Kama sio waamini, basi utapaswa kurudia yale masomo ya kwanza matatu yahusuyo wokovu.
3. Omba. Roho Mtakatifu ni mwalimu wako. Mwache akuongoze

jinsi uwezavyo kufundisha ukweli wa somo hili.

4. Jifunze somo. Watu wengi ambao hawajakua Kikristo huwa na woga wa kupoteza wokovu wao. Hili ni somo la muhimu la kuwahakikishia na kuwawezesha kuelewa maisha yao katika Kristo. Soma yale yaliyosemwa katika kitabu cha wanafunzi na kitabu cha waalimu.

5. Uwe na utaratibu wa mpango wa kufundishia. Muda utakaokuwa na wanafunzi ni mfupi sana. Kwa hivyo unapaswa kuupangia kwa uangalifu. Fikiria kuhusu muda utakao tumia kwa:

- a) kulirudia somo lililopita.
- b) kutoa utangulizi wa somo la leo.
- c) kufundisha somo lenyewe.
- d) kutumia ukweli wa somo hilo.
- e) kufundisha kifungu cha kukumbuka.
- f) kujibu maswali ya "kazi ya kufanya".

Soma Warumi 8:1-4. Aliyemwamini Kristo ana uhusiano mpya. Alikuwa akihukumiwa na sheria ya Mungu kabla ya kuokoka. Kila mmoja amefanya dhambi na anayo adhabu ya kifo. "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti..." (Warumi 6:23) Kristo aliwalipia deni la mauti wote watakaomwamini. Kwa hivyo, ye yote amwaminiye Kristo kwa ajili ya msamaha wa dhambi huanza ushirika mpya na sheria za Mungu. Yuko huru

Kulingana na mahitaji ya sheria. Hatahukumiwa kwa ajili ya dhambi zake kwa sababu amesamehewa. Mwamini huishi maisha yake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu aishiye ndani yake. Roho humsaidia kuishi katika ushindi kwa sababu yu katika Kristo na Kristo yu ndani mwake.

Soma Wagalatia 2:19-20. Kama waamini tuko huru kutoka kwa hukumu ya Mungu ya dhambi na tuko huru kutoka kwa uwezo wa dhambi na mauti. Kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo ndio ukweli muhimu wa Injili. Tunaokolewa kwa imani katika Kristo kwa sababu alitufia. Tunaishi kwa imani katika Kristo kwa sababu anaishi ndani yetu. Kristo alitushindia nguvu za shetani alipofufuka katika wafu. Ushindi wake ndio ushindi wetu. (Soma 1 Yohana 3:8)

Tunapaswa kumfanya Kristo Bwana wa maisha yetu ikiwa tunataka kufurahia ushindi huu katika Kristo. Kwa hivyo ni lazima tufanye mambo mawili:

1. kufia nafsi yetu, na
2. kumtii Kristo.

“Kusulubiwa” inamaanisha kumwachia Kristo haki ya kumiliki maisha yetu. Ni lazima Kristo awe wa kwanza katika kila sehemu ya maisha yetu: katika mipango yetu, hali ya kuishi, kazi, mawazo, nia, na kusudi. Tunapaswa kumpendeza yeye kuliko kitu kingine cho chote.

Maisha yetu mapya ni “katika Kristo”. Kwa hivyo tunaweza kuishi katika ushindi wa dhambi kwa sababu Kristo anaishi ndani yetu. Yeye ndiye

nguvu zetu. Hatuwezi kumshinda Shetani anapotujaribu, lakini Kristo anaweza. Tunayo njia katika uwezo wa Kristo na haki yake. Tunadai haki hizi za kupigana na Shetani katika imani.

Soma Warumi 8:35-39. Hatupaswi kuogopa kwa sababu hatuwezi kutenganishwa na Mungu. Vijana wengi huwa na wasiwasi wa kupoteza wokovu wao. Huongea kuhusu kuokoka na baadaye kuupoteza wokovu kwa ajili ya dhambi. Haiwezekani kamwe kama kweli wameokoka, na kuzaliwa mara ya pili, hawawezi kupoteza uzao wao. Yesu alisema kwamba, “Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe, wala hakuna atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu. Mimi na Baba tu umoja” (Yohana 10:28-30).

Hupaswi kuogopa kifo, wakati ujao, vitu vya mbinguni, au duniani au chini ya dunia. Tuko salama KATIKA KRISTO. Hakuna liwezalo kututenganisha na upendo wake. Tunapaswa kuiamini ahadi hii na kuidai kwa imani.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia watoto kufahamu kwamba waamini wanaweza kuishi maisha ya ushindi kwa sababu Kristo anaishi ndani yao nao wanaishi ndani yake.

KULIFUNDISHA SOMO

Andika neno USHINDI kwa herufi kubwa ubaoni au kwenye karatasi kubwa.

Uliza maana ya neno “ushindi”. Zungumzia njia ambazo ushindi hutuletea furaha.

Wakumbushe wanafunzi baadhi ya wanamichezo ambao wameiletea nchi yao sifa na kuifanya ijulikane.

Uliza: Je, watu walifanyaje baada ya shindano hilo?

Wasimulie hadithi ya Wilma Rudolph ambayo imo katika vitabu vyao. Waambie jinsi alivyoshinda matatizo mengi na akajulikana sana katika ulimwengu wa michezo. Kipchoge Keino, wa Kenya, alishinda mbio hizo hizo wakati mwingine wa michezo ya Olimpiki.

Sema: Wilma alifanya kazi kwa bidii kila siku ili awe mshindi. Kristo anawataka wafuasi wake pia kuwa washindi. Ushindi anaotaka tuupate ni wa muhimu sana kuliko ule wa ulimwengu wa michezo. Ni ushindi wa nafsi zetu, dhambi na Shetani. Hebu tuone kwa nini tupate ushindi huu.

Andika maneno haya ubaoni: KWA NINI TUISHI KATIKA USHINDI.

Mwambie mshiriki mmoja asome Warumi 8:1-4.

Sema: Sababu ya kwanza ya mwamini kuishi katika ushindi ni kwamba yuko huru kutoka kwa hukumu ya Mungu. (Andika ubaoni hivi, HURU KUTOKA KWA HUKUMU YA MUNGU.) Mtu huwa chini ya sheria ya Mungu hadi ampokeapo Kristo. Dhambi zake humletea hukumu ya kifo. Hata hivyo, Kristo alikufa msalabani na akalipa deni la dhambi. Kwa hivyo, wote wamwaminio hufanywa huru kutokana na adhabu ya dhambi.

Uliza: Je, hakimu humwambiaje mfungwa anapoachiliwa apatikanapo bila hatia? (Uko huru, umesamehewa, na kufunguliwa).

Sema: Hivyo ndivyo Kristo ametutendea. Tungeadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu, lakini Kristo ametuweka huru. Hii inamaanisha kwamba Mungu hatatuhesabia tena dhambi hiyo.

Mwambie mshiriki mwingine asome Wagalatia 2:19-20. Ushirika wa mtu na Kristo hubadilika wakati anapomwamini kwa ajili ya msamaha wa dhambi. Yeye huwa katika Kristo na Kristo huwa ndani yake.

Uliza: Je, kusema “kusulubiwa pamoja na Kristo” ina maana gani? Eleza kwamba mambo mawili hufanyika unapo sulubiwa pamoja na Kristo: (1). kufia nafsi yako, na (2). kumtii Kristo.

Sisi kama wanadamu huwa tunataka kutenda jinsi tutakavyo na kujitawala maishani. Hata hivyo, watu walikufa kwa kusulubiwa. Ni lazima tufie nafsi zetu ili Kristo aweze kutawala maisha yetu. Jambo hili sio rahisi. Inamaanisha kujinyima haki zetu na kumfanya Kristo awe wa kwanza. Jambo la pili ni kwamba ni lazima tumtii Kristo. Tunaonyesha kuwa sisi ni wanafunzi wa Kristo kwa kumtii.

Waambie wanafunzi kadhaa kusoma vifungu vifuatavyo: Yohana 14:21, Yohana 14:23-24; Yohana 15:10.

Soma tena Wagalatia 2:19-20 na uandike ubaoni sababu ya pili ya kuishi katika ushindi. Andika hivi, KUWA HURU KUTOKA KWA UWEZO WA DHAMBI NA MAUTI.

Sema: Hakutakuwepo na wakati ambapo shetani ataacha kutujaribu na kutufanya tukose kutii. Hata hivyo, Kristo alimshinda Shetani alipokufa msalabani na kufufuka. Shetani sasa ameshindwa.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome 1 Yohana 3:8. Kristo ametushindia nguvu za Shetani. Sisi huyakabili majaribu na shida kwa uwezo wa Kristo aishiye ndani yetu, wala sio uwezo wetu wenyewe. Ushindi wake huwa ushindi wetu.

Mwambie mwingine asome 1 Yohana 4:4. Kristo aishiye ndani yetu ni mkuu kuliko Shetani aishiye ulimwenguni. Hutupa uwezo wa kushinda udhaifu wote katika Roho Mtakatifu.

Soma Warumi 8:35-39. Sababu ya tatu ya kuishi katika ushindi ni kwamba hatuwezi kutenganishwa na upendo wa Mungu.

Andika ubaoni UHURU WA WOGA.

Sema: Waamini wengi huwa na wasiwasi ya kwamba wanaweza kupoteza wokovu wao. Wengine huogopa kufa. Hata wengine huogopa kila kitakacho tendeka kwao wakati ujao. Vifungu hivi vimejaa tumaini. Hatupaswi kuogopa tukiwa katika Kristo.

Mungu hatufanyi kutopata mateso. Hutumia mateso ili kutukuza kiroho. Naye hutupa uwezo wa kuyashinda. Kifungu cha 37 kinasema hivi, "Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda." Nafasi yetu iko katika Kristo na hatuwezi kutenganishwa na upendo wake.

Rudia yale mambo ambayo Kristo ametufanyia:

1. Ametuweka huru kutoka kwa uwezo wa dhambi kwa sababu alikufa kwa jili yetu.
2. Ametuweka huru kutoka kwa uwezo wa dhambi na mauti kwa sababu anaishi ndani yetu.
3. Ametuweka huru kutoka kwa woga kwa sababu hakuna kiwezacho kututenganisha na upendo wake.

Sema: Haya ndio yale ambayo Kristo ametufanyia. Sisi tunapaswa kufanyaje?

Uliza: Je, unafikiria inawezekana kwako kuishi maisha ya ushindi? (Ngojewa majibu.)

Uliza: Je, ni pingamizi zipi ziwezazo kukufanya kutoona ushindi wa dhambi maishani mwako? (Kutotaka kuacha tabia mbaya, udhaifu, kutoamini ahadi za Mungu)

Uliza: Je, unawezaje kuufahamu ushindi huu? (Kuomba msamaha na kumruhusu Kristo kuwa Bwana wa maisha yako.)

Omba. Mshukuru Mungu kwa ajili ya ushindi tulionao katika Kristo. Mshukuru kwa sababu hakuna tatizo au jambo ambalo hawezi kulishinda. Mshukuru kwa ajili ya nafasi yetu kwake ambayo hutufanya tuishi maisha ya ushindi.

KAZI YA KUFANYA

Soma maandiko yafuatayo na ujibu maswali yahasuyo USHINDI KATIKA KRISTO.

1. Je, Kristo ananitaka niishi maisha yapi? (1 Yohana 5:4) **MAISHA YA USHINDI.**

2. Je, nitakuaje na imani? (Warumi 10:17) **KWA KUSIKIA NENO LA MUNGU.**

3. Je, Mungu hunipaje ushindi maishani mwangu? (1 Wakorintho 15:57) **HUNISHINDISHA KUPITIA KWA BWANA WETU YESU KRISTO.**

4. Kristo aishiye ndani yangu anahusuje uwezo wa Shetani juu yangu? (Wagalatia 2:20) **HANA UWEZO KWA SABABU KRISTO ANAISHI NDANI YANGU.**

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo” (1 Wakorintho 15:57).

Wape wanafunzi hao muda wa kuandika ombi lao katika vitabu vya wanafunzi. Wahimize ili waweze kuandika dhambi au pingamizi yo yote wanapotaka Kristo awashindie. Ombea jambo hilo.

WAKATI WA MWISHO

Imbeni pamoja kifungu cha wimbo usemao, “Ushindi katika Kristo.” Kama hawafahamu wimbo huu, mnaweza kuimba wimbo mwingine unaosisitiza kazi ya ushindi wa Kristo kwetu.

Malizia kwa kuwaombea washiriki hao ili wiki hii wapate ushindi wa Kristo maishani mwao.

SURA YA TANO

KUKUA KATIKA KRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Waefeso 4:1-7
KUJIANDAA KUFUNDISHA

Washiriki wako sasa wanakua. Wanakua kimwili na kimaarifa. Ni muhimu kwao kukua kiroho pia.

Vijana huwa na maswali mengi na nguvu nyingi. Wanataka kufahamu yale yafanyikayo ulimwenguni na kujifahamu wenyewe. Yale wanayofikiria kuwa ni muhimu huwa yanabadilika.

Wakati huu wa mabadiliko vijana hutaka kuona mifano iliyowekwa na wazima, au watu “waliofanikiwa kutimiza”. Hutaka kuiga maisha ya mashujaa. Wanaweza kujiita mtu waliyemsikia redioni, waliyemwona katika televisheni au katika sinema. Ni muhimu kwao kuchagua mtu aliye Mkristo.

Wewe kama mwalimu wao unapaswa kuwa mfano kwao na pia kiongozi wa kiroho ambaye wanapaswa kuiga. Uko katika hali ambayo inaweza kugeuza fikira zao na uchaguzi wao. Unapaswa kuwa mwalimu anayekua kiroho ili uwe mfano mzuri. Washiriki hao wayaangalie matendo yako. Je, ni nini waonacho kizuri katika maisha yako ya Kikristo ambacho wangepurahia kukiiga?

Julize mwenyewe maswali haya:

1. Ninafanya nini ili nikue kama Mkristo?
2. Je, ni vipi ambavyo mimi ni mfano mzuri kwa wanafunzi wangu?

3. Naweza je kuwasaidia kukua kiroho?

Sura ya kwanza tatu za Waefeso zinafundisha imani ya Wakristo. Nazo tatu za mwisho zafundisha kuhusu hali na matendo ya Mkristo. Vifungu vya somo hili vinahusu hasa umoja wa Wakristo.

Kanisa la Efeso lilikuwa na washiriki wa Kiyahudi na wale wa Mataifa. Walikuwa na shida ya kushirikiana kwa kazi. Paulo hakutaka kuona kanisa hilo likiwa limegawanyika. Aliwataka wauonyeshe ulimwengu kuwa wana umoja katika Kristo.

Kifungu cha 1 hadi 3. Paulo alianza kwa kusema kwamba alikuwa mfungwa wa Bwana. Neno “mfungwa” lina maana mbili:

(1) Hasa, Paulo alikuwa amefungwa alipoandika barua hii. (2) Ali-maanisha pia kwamba, alikuwa chini ya mamlaka ya Kristo jinsi mtumwa akuwapo chini ya mamlaka ya Bwana wake.


Paulo aliwahimiza waamini kuishi maisha yanayolingana na mwito wao wa Kikristo. Ushirika wao kama waamini uliudhihirishia ulimwengu kwamba walikuwa pamoja katika Kristo. Walikuwa na kiongozi mmoja - Kristo. Walikuwa na kazi moja - kumtambulisha Kristo.

Somo hili laweza kusaidia kanisa la sasa. Makanisa mengi ya Afrika yana watu wa makabila mbali mbali na asili tofauti. Umoja hudhihirishwa wakati

Wakristo wapendanapo na kufanya kazi pamoja. Ujumbe wa Kristo hautaeleweka kwa wasiowaamini ikiwa Wakristo hawataelewana, au kuwa na migawanyiko na kukataa kufanya kazi pamoja.

Paulo aliandika kwamba kulikuwa na hali au neema za Wakristo ambazo wanapaswa kuzikuza. Baadhi yazo ni:

1. Uvumilivu. Wakristo wanapaswa kwanza kuwafikiria wenzao.
2. Unyenyekevu. Yesu alikuwa mnyenyekevu lakini hakuwa mdhaifu. Unyenyekevu unaonyesha kwamba unatawaliwa kuongozwa. Ni picha ionyeshayo utiifu na adabu nzuri.
3. Ufadhili: Waamini wanapaswa kuwa wafadhili kwa wenzao jinsi Kristo alivyokuwa mfadhili kwao. Hawapaswi kulipiza kisasi, bali kuonyesha upendo.
4. Ustahimilivu. Hawapaswi kuwa wakali kwa wenzao. Wanapaswa kuzuia hasira zao.
5. Amani. Mwamini anapaswa kwanza kuwa na amani na Mungu, ndipo awe na amani na wenzake.



Amani ni karama ya Mungu ambayo mwamini huipata awapo na amani ndani yake.

Kifungu cha 4 hadi 7.

Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani ya watu ili kuondoa hitilafu na kuleta umoja. Ni lazima Wakristo wahifadhi umoja huu. Paulo anatoa orodha ya mambo saba ambayo Wakristo wanapaswa kuwa na umoja.

1. Mwili mmoja ni picha ionyeshayo ushirika wa Wakristo. Kila mwamini ni sehemu ya mwili wa Kristo.
2. Roho mmoja ni-Roho Mtakatifu. Wakristo wana Roho aina moja. Roho Mtakatifu hudhihirisha kuwepo kwa Mungu kati ya watu wake.
3. Tumaini moja ni lile lidhihirishalo ahadi ya kurudi tena kwa Kristo.
4. Bwana mmoja ni Yesu Kristo. Kuna Mwokozi mmoja tu, na hakuna mwingine ye yote ambaye Wakristo wanapaswa kumtegemea.
5. Imani moja inamaanisha kwamba washiriki wote wa kanisa huokolewa kwa kumwamini Yesu Kristo.
6. Ubatizo mmoja huhadhihirisha kwamba kila Mkristo anamwendea Yesu kwa imani. Ubatizo hufuata wokovu na hufanywa kwa kulitii agizo la Kristo. Ubatizo hauokoi. Bali ni ishara ionyeshayo kukiri kwa yale yaliyofanyika ndani yako.
7. Mungu mmoja na Baba mmoja kwa wote inamaanisha kwamba Mungu ndiye anayetawala. Wakristo wanaye Mwumba mmoja na Mwokozi ambaye ni Baba wa upendo.

Wakristo wote ulimwenguni wameunganishwa kama jamaa moja. Tunaweza kuwa na umoja kwa sababu tuna Baba mmoja anayetawala na kuongoza jamaa hiyo. Wakristo hukua wanapokuwa na umoja wa kusudi na mwongozo. Sisi kama jamaa moja, ni mali ya wenzetu na pia tunawahusu wenzetu. Tunategemeana. Mwili wa Kristo hukua wakati kila mshiriki akuapo. Washiriki hukua wanapojifunza Neno la Mungu na kuhudumu katika upendo wake.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza washiriki katika kutambua njia ambazo wanaweza kukua katika neema za Kikristo.*

KULIFUNDISHA SOMO

Anza kwa kusimulia hadithi ya Mazula iliyoko katika vitabu vya wanafunzi. Chora ubaoni picha ya fimbo ya kupimia, kama ile ifuatayo.

Uliza: Je, ungekuwa na kipimo kipi ikiwa jina lako lingeitwa ili upimwe jinsi ulivyokua kiroho? (Eleza kwamba hii ilikuwa ndoto tu, lakini ni mfano utufanyao tufikirie jinsi tulivyokua.)

Uliza: Je, mwamini huanza wakati gani kukua kama Mkristo? (Anapomwamini Kristo kama Mwokozi wake.)

Uliza: Je, wote walio Wakristo hulingana kwa kukua? (La, hiyo hutegemea yale Mkristo afanyayo ili akue. Kuna uwezekano wa kubakia tu pale pale bila kukua zaidi.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waefeso 4:1-3.

Sema: Paulo aliandika juu ya baadhi ya neema za Wakristo au hali ambazo waamini wanapaswa kukua.

Uliza: Taja neema zilizo rodheshwa katika vifungu hivi. (Ziandike ubaoni wanapozisema.)

Waonyeshe lile neno “Unyenyekevu au uvumilivu”. Waelezee linamaanisha kwamba Wakristo wanapaswa kuwafikiria watu wengine kwanza kuliko nafsi zao. Mwambie mtoto mwingine asome Wafilipi 2:3. “Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenzake kuwa bora kuliko nafsi yake.”

Uliza: Je, mnaweza kutaja njia ambazo mnaweza kuwahesabu wenzenu kuwa bora kuliko nafsi zenu? (wape muda wa kujadiliana na kujibu.)

Waonyeshe neno “upole” uliloliandika ubaoni.

Sema: Yesu alikuwa mpole na Biblia inasema kwamba Musa alikuwa mpole pia (Hesabu 12:3). Je, inamaanisha nini kuwa mpole? (Yasikize majibu yao.)

Uliza: Ikiwa mtu ni mpole, je, hiyo humaanisha kuwa yeye ni mdhaifu? (La, inamaanisha uwezo wa mtu huyo unatawaliwa.)

Waambie wanafunzi hao wamfikirie mwana farasi ambaye hajawahi kufundishwa cho chote. Eleza kwamba huwa mwenye nguvu, lakini hawezi kuongozwa.

Mwana farasi aanzapo kufundishwa hujifunza kutii. Hatimaye huanza kutumika kwa sababu nguvu zake zote

na uwezo huwa unaongozwa na yule anayemfunza.

Hatumfikirii Yesu kuwa mpole alipowafukuza wanunuzi kutoka hekaluni. Hali tunapofikiria jinsi alivyomchukua mtoto mikononi mwake na kumbariki, huwa tunamwona kuwa ni mpole. Yesu alikuwa chini ya utawala wa Baba yake. Tunapaswa kuwa wapole ili tuishi chini ya utawala wa Kristo.

Waonyeshe lile neno "Uvumilivu au Ufadhili" uliloandika ubaoni.

Sema: Sisi tumezoea kulipiza kisasi tunapokosewa na wenzetu. Hivyo sio kuvumilia.

Uliza: Je, inamaanisha nini kuwa mvumilivu? (Ngojewa majibu. Baadaye eleza kwamba kuvumilia ni kustahimili shida zote bila kulipiza kisasi)

Sema: Yesu huvumilia tunapokosa, nasi tunapaswa kuvumilia wenzetu wakosapo.

Waonyeshe lile neno "ustahimilivu" uliloandika ubaoni.

Sema: Kuna watu ambao hatupendi kukaa nao jinsi tunavyofurahia tukiwa na wengine. Kuna watu wenye hali mbali mbali. Ustahimilivu ni neema ya kuwakubali wengine jinsi walivyo. Pengine hatuwezi kufurahi tukiwa pamoja nao, lakini huwa tunawaonyesha upendo wa Mungu.

Uliza: Unaweza kumfikiria mtu ambaye humpendi? Sasa hebu fikiria baadhi ya matendo uwezayo kufanya ili uwaonyeshe upendo. Ukifanya hivyo utaweza kuikuza neema ya ustahimilivu maishani mwako.

Waonyeshe neno "amani" ulioandika ubaoni.

Uliza: Inamaanisha nini kuwa na amani? (Kuishi kwa umoja, mapatano au bila kugombana)

Uliza: Je, inamaanisha kuishi bila matatizo? (La, inamaanisha kuwa na roho wa utulivu hata ingawa una shida.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wafilipi 4:6-7.

Uliza: Je, kifungu hiki kinasema amani hupatikana wapi? (Kwa Mungu)

Sema: Amani ni karama ya Mungu kwetu. Hata hivyo, ni lazima mtu awe na ushirika mzuri na Mungu kabla ya kupata amani ya kweli. Hatimaye anaweza kuishi kwa amani na wenzake.

Uliza: Je, una amani ya kweli? Je, una jambo lo lote ambalo unapaswa kufanywa ili uwe na ushirika mwema na Mungu? Mungu anataka wafuasi wake waishi kwa amani naye pamoja na wenzao.

Mwambie mshiriki mmoja asome Waefeso 4:4-7.

Sema: Paulo alieleza kuhusu neema za Wakristo zilizohitajika kanisani. Yalikuwa mambo ambayo washiriki walipaswa kuyakuza. Mwishowe aliwaambia jinsi washiriki walivyo "umoja" katika Kristo.

Sema: Tajeni jinsi Wakristo walivyo na umoja. (Ngojewa majibu)

Eleza kwa kifupi maana ya kila mojawapo ya maneno haya:

Mwili mmoja - Kanisa ni jamaa ya kiroho, nao ni mwili wa Kristo.

Roho mmoja - Waamini hupata Roho Mtakatifu wanapompokea Kristo maishani mwao.

Tumaini moja - Tumaini la waamini ni kurudi tena kwa Kristo.

Imani moja - Tunaokolewa kwa imani katika Kristo.

Ubatizo mmoja - Ubatizo ni ishara ionyeshayo imani yetu katika Kristo.

Mungu mmoja na Baba - Mungu ndiye anatawala kila kitu na yuko ndani ya kila mwamini.

Sema: Makanisa mengi huwa na matatizo na sababu mojawapo iletayo shida ni kuwa Wakristo hawakui kamwe. Hawakuzi neema za Kikristo ambazo huleta umoja. Kuna watu wengi wazima ambao wangali wachanga katika Ukristo wao. Jambo hili linahuzunisha sana. Anaweza kulinganishwa na mtoto ambaye hakui kamwe. Nalo si jambo la kawaida.

Sema: Neema za Kikristo ambazo tumejifunza leo ni dhihirisho la kukua kwetu kama Wakristo. Roho Mtakatifu aishiye ndani yetu hutusaidia kukuza neema hizi ambazo huleta umoja katika mwili wa Kristo.

Uliza: Je, ni mambo yapi unayoweza kufanya ili ukue kama Mkristo? (Kusoma Neno la Mungu, kuomba, kushiriki pamoja na waamini, kushuhudia.)

Sema: Fikiria jambo ambalo utafanya wiki hii litakalo kusaidia kukua kama Mkristo. Liandike kwenye karatasi na uliweke mahali ambapo utalionga kila siku. Liache likukumbushe jambo ambalo litakuhimiza kukua kama Mkristo.

KAZI YA KUFANYA

Mazula aliota kwamba alikuwa akipimwa jinsi alivyokua kiroho. Je, utakuwa na urefu upi ikiwa nawe utapimwa? Jipime kwa kipimo cha 1-5.

Huwa mpole kwa wenzangu.

Huwasamehe wenzangu mara tu wanikoseapo.

Hutamani kukua Kiroho.

Husoma Biblia yangu kila siku na kuomba.

Nina uhusiano mwema na jamaa yangu.

Nakubaliana na wenzangu jinsi walivyo.

Naishiriki imani yangu na wenzangu.

Natumia karama na vipawa vyangu kanisani.

Huwasaidia walio na mahitaji.

Sijibu kwa ukali wale wanikoseao.

Nimemfanya Kristo kuwa wa kwanza, halafu wengine na mimi mwenyewe wa mwisho.

Ninajaribu kuishi kwa amani na wenzangu.

Naonyesha upendo kwa wale ambao sifurahii nikiwa pamoja nao.

Waefeso 4:4-7 inatuambia sababu ziwafanyazo washiriki kuwa na umoja katika ushirika wao. Soma maandiko hayo na ujaze nafasi zilizoachwa.

Kuna MWILI mmoja na ROHO mmoja, kama na mlivyoitwa katika TUMAINI moja la wito wenu, BWANA mmoja, IMANI moja, UBATIZO mmoja, MUNGU mmoja, naye ni BABA wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo" (2 Petro 3:18).

WAKATI WA MWISHO

Uliza: Je, mnaweza kutaja baadhi ya neema za Kikristo ambazo huleta ukuzi?

Uliza: Kifungu chetu cha kukumbuka kinatuhimiza tukueje?

Sema: Tutakua katika neema na maarifa ya Bwana iwapo tutakuza hali yetu ya Ukristo baina yetu.

Taja jinsi tuwezavyo kukua katika maarifa ya Kristo. (kwa kujifunza Biblia, kuomba, kushiriki na waamini, kushuhudia)

Ombeni pamoja. Mwombe Mungu awaonyeshe wanafunzi hao jinsi ya kukua. Mshukuru kwa ajili ya ukweli aliofundisha katika somo hili.

SURA YA SITA

LENGO LA MAISHA

MASOMO YA BIBLIA: Wafilipi 3:12-21

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Vijana huwa wanaambiwa mara kwa mara kwamba wao ni “wadogo sana”. Huwa hawakubaliwi kuenda po pote watakapo, au kutokubaliwa kuoa, au kutafuta kazi na pia huambiwa kwamba hawawezi kusikizwa na wazee. Haya yote hubadilika kulingana na wakati. Wakuapo wazima hukubaliwa kuoa, kwenda kazini na wazee huwasikiliza wasemapo.

Kuna hitaji la kukua katika maisha ya Kikristo. Hii haitokei unapokuwa mzee, lakini yaweza kuwa hivyo. Mkristo hukua katika imani anapokuza ushirika wake na Yesu Kristo. Kila mwamini anapaswa kuwa na lengo la kukua.

Paulo aliwaandikia Wafilipi kwamba hakujifikiria kama yeye amekua kikamilifu. Kulikuwa na ukweli ambao alitakiwa kujifunza. Lengo la Paulo lilikuwa kujifunza mengi kuhusu Kristo na kueneza habari yake kwa wote. Kazi yake ilidhihirisha kwamba alilifuata hasa lengo lake.

Utatakiwa kufanya mambo yafuatayo unapotayarisha somo hili:

1. Mwombe Roho Mtakatifu akufundishe jinsi uwezavyo kushiriki ukweli wa somo hili.
2. Soma vifungu vya Biblia. Tafuta maana ya maneno ambayo huelewi.
3. Soma kwa uangalifu kitabu cha waalimu pamoja na somo katika kitabu cha wanafunzi.

4. Waombe wanafunzi wa darasa lako. Fikiria jinsi wakuavyo kiroho na jinsi uwezavyo kuwahimiza ili wakue kama Wakristo.

(Kifungu cha 12 hadi 15) Paulo alikuwa ametosheka na Kristo, lakini hakuwa amejitosheleza mwenyewe. Angejichukua kwa hali ya juu kwa sababu ya kurithika kwake na yote aliyotekeleza. Hata hivyo, hakukubali kujidanganya. Hakuchukua ushindi wake kuwa wenye maana yo yote.

Neno hili “mkamilifu” lililo katika kifungu cha 12 linamaanisha “kukua kabisa”. Katika kifungu cha 10 ametumia neno “kumjua Kristo” kama jambo lililo la umuhimu kwake. Kwa hivyo alikuwa akisema kwamba hakuwa amemjua Kristo kikamilifu, hali hakuwa mfuasi wa Kristo kwa muda mrefu.

Paulo hakufikiria yaliyopita. Kulikuwa na matendo maishani mwake ambayo hakuyafurahia. Alikuwa amewatesa waamini na kutoamini kwamba Yesu ndiye Masihi. Hangekubali matendo yake maovu au ushindi wake uzuie kutoendelea kwake.

Paulo alikaza mwendo kulifikia lengo lake. Alikuwa ameisha wahubiria watu wengi na kuanzisha makanisa kadhaa. Lakini hakutosheka kwamba baadhi yao walikuwa wamemwamini Kristo nao walikua kiroho. Kulikuwa na wengi ambao hawakuwa wamesikia ujumbe wa Injili. Hakuwa ameimaliza kazi yake.

Usemi huu wa “kukaza mwendo kwa kulifikia lengo” hutumiwa sana na wana michezo. Huonyesha picha ya mkimbiaji anayejikaza ili afikie kamba. Hutumia nguvu zake zote ili aifikie kamba ambayo ndilo lengo lake.

Tuzo lake lilikuwa kumpendeza Kristo. Maana ya “mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu,” ni kutimiza mwito wa Mungu maishani mwake Kristo alikuwa amemgusa na alimtaka aishi na kumfanyia kazi. Mwito wake ulikuwa kuwafanya Mataifa kuwa wanafunzi wa Kristo. Ulikuwa mwito mkuu kwa sababu ulitoka kwa Kristo mwenyewe na sio mwanadamu.

Wakati wa Paulo, washindi wa mchezo wa Olimpiki walipewa tuzo ya maua yaliyosokotwa kama kata na kuvalishwa shingoni. Lakini siku hizi washindi hupewa medali ya shaba au dhahabu. Paulo alikuwa akitarajia kutuzwa baada ya kifo chake. Halingeisha wala kuzeeka. Lilikuwa tuzo la milele ambalo angepewa kwa kuwa mwaminifu katika kutekeleza kazi aliyopewa na Mungu.

Kifungu cha 17 hadi 21. Mnifuate mimi. Paulo hakuwa anajivuna aliposema, “Mnifuate mimi.” Alikuwa mwalimu naye alilikubali jukumu hilo lake. Alijua kwamba Mwalimu anapaswa kuwa mfano kwa wanafunzi wake. Alikuwa amefuata mwito na kusudi la Kristo na ingekuwa vizuri kuiga utii wake.

Wanafunzi wako wanaangalia jinsi unavyoishi. Wanajifunza mengi kwa kukuangalia kuliko yale unayo-fundisha. Je, unaishi maisha uwezayo

kusema, “Nifuateni mimi jinsi ninavyokua kiroho?”

Kulikuwa na maadui wa msalaba. Paulo aliandika ka huzuni nyingi kuhusu watu wa kanisa la Filipi ambao walikuwa wakidhihaki jina la Kristo. Walitaka kujipendelea wao wenyewe. Walishughulikia hasa chakula na mambo ya ulimwengu, na wakajivunia vitu ambavyo kwa kweli wangevionea haya. Onyo hili ni letu pia. Je, huwa tunashughulikia mambo yale ambayo ni muhimu? Au huwa tunashughulikia mambo yale ambayo yatatufurahisha wakati huo tu?

Mbinguni ndiko nyumbani kwetu. “Wenyeji wetu” inamaanisha “uraia wetu” au “nyumbani kwetu”. Paulo alikuwa akisema kwamba tuna muda mfupi hapa duniani. Nako siko nyumbani kwetu. Tuko tu duniani kwa miaka michache, lakini tutaishi milele kule nyumbani kwetu ambako ni mbinguni. Huko tutapewa miili mipya na Kristo. Ataweza kutufanyia hivi kwa sababu ana uwezo wote, na vitu vyote viko chini ya mamlaka yake.

Muhtasari: Lengo la Paulo lilikuwa kumjua Kristo na kueneza habari zake. Aliwahimiza waamini:

-kutoacha kujaribu.

-kutoangalia yaliyo nyuma.

-kufuata mfano wa wale walio waaminifu.

-kukaza mwendo ili walifikie lengo la kukua kiroho.

-wakumbuke kwamba nyumbani kwao ni mbinguni watakakoishi na Yesu.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi katika kuchagua lengo la maisha la kukua Kikristo na kutambua jinsi ya kulifikia lengo.*

KULIFUNDISHA SOMO

Mpe kila mwanafunzi karatasi na uwaambie wafanye kazi ifuatayo:

1. Waandike jambo moja lililofanyika kwao ambalo walilifurahia.
2. Waandike jambo moja lililofanyika kwao ambalo hawakulifurahia. (Unaweza kujadiliana tu na wanafunzi ikiwa hakuna karatasi. Wahimize waongee kuhusu walivyopita mtihamu wao, jinsi walivyosumbuliwa na mwalimu kutokuelewana au ushindi waliopata.)

Wasimulie hadithi ya mwanafunzi aitwaye Jim. Jim alifurahia alipopita mtihamu yake. Alipenda uamuzi wa waalimu na akafurahia kuwa wa kwanza kila mara. Alipita mtihamu wake wa mwisho vizuri sana. Alikuwa na uhakika wa kupata nafasi katika shule mojawapo nzuri pale nchini.

Mwalimu wake wa “nyumbani” alikuwa Mkristo. Alifurahia kazi ya Jim, lakini alisema kwamba Jim “alijisifu sana” kwa wenzake.

Siku moja mwalimu wake alimwita kwa majadiliano mafupi. Akamwambia, “Jim, wewe ni mwanafunzi mzuri sana. Umetufanya tujivune sana hapa shuleni. Tunajua kwamba ukizidi kufanya kazi kwa bidii utafanikiwa sana. Hata hivyo, kuna jambo ambalo limetuhusu sana.”

Jim akamwuliza, “Je, nimekosa nini?”

Mwalimu akamwambia, “Hujakosa, bali ni tabia yako. Unajivunia sana kufaulu kwako na hili linaweza kuwa tatizo kubwa katika maisha yako ya baadaye. Tabia yako ya kusema, ‘mimi ni bora zaidi’ yaweza kukufanya usiweze kupita vizuri wakati mwingine. Na vile unavyoendelea ndivyo mambo yanavyoanza kuwa magumu. Pengine Mungu ana mpango muhimu nawe wa kusaidia katika kujenga nchi yako. Mungu anakutaka utumie maarifa na uwezo aliokupa kwa kutenda yaliyo mema.”

Jim alibaki kimya kwa muda mfupi. Hatimaye akasema, “Nimefurahi kwa sababu umeniambia jinsi nilivyotenda. Sikufikiria kwamba Mungu anaweza kunitumia. Sasa nitafanya kazi kwa bidii, na kwa uwezo wangu wote.”

Uliza: Ni nani awezaye kutuambia wema aliotenda ambao aliufurahia sana? (Ngojea majibu)

Uliza: Nataka mmoja wenu atuambie tatizo ambalo alikabiliana nalo hivi karibuni. (Wape muda wale ambao wangependa kueleza.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wafilipi 3:12-15.

Uliza: Paulo alisema juu ya kufikiria yale yaliyopita. (Tusiyaifikirie kamwe.)

Uliza: Je, kuna ubaya gani tukiyafikiria? (Hatuwezi kuendelea mbele.)

Uliza: Je, Jim, alikosaje? (Alijivunia sana kupita kwake.)

Ongea kuhusu ukumbukaji wa makosa uliyofanya, au ushindi uliopata waweza kuzuia maendeleo.

Uliza: Paulo alifikiriaje kuhusu yale aliyokuwa ametenda? (Mwambie mwanafunzi asome kifungu cha 7 na 8. Aliyahesabia kuwa ni hasara.)

Uliza: Paulo alikuwa na lengo lipi? (La kupata thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.)

Eleza kuwa maana yake ni kwamba Mungu alimwita Paulo na kumpa kazi ya kufanya. Ulikuwa mwito wa Mungu wala sio wa mwanadamu. Angelifikia lengo la kumjua Kristo na kumjulisha kwa wengine ikiwa angekuwa mwaminifu.

Uliza: Je, ni thawabu au tuzo lipi ambalo Paulo alizungumzia? (Kutimiza kazi ya mwito wa Mungu.)

Eleza kwamba katika wakati wa Paulo watu waliifahamu michezo ya Olimpiki. Mshindi alipewa tuzo la maua. Paulo hakutaka kupewa tuzo itolewayo na mwanadamu bali ile itolewayo na Kristo. Ingetolewa baada ya kifo chake nayo ingekuwa ya kudhihirisha uaminifu wake wa kutimiza kazi aliyopewa. Tuzo hiyo haingechakaa wala kuzeeke. Angepewa uzima wa milele.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wafilipi 3:16-19. Paulo aliwataka waamini kuyafikiria mambo yajayo.

Uliza: Ni mambo yapi aliyosema watende ili kuchuchumilia yaliyo mbele. (Kifungu cha 16: kuenenda katika yale waliyojifunza, kifungu cha 17: kufuata mfano wa wale waliokua katika imani, kifungu cha 18: kujihadhari na wale watakao kujiletea sifa, kifungu cha 19: wasipande mambo ya dunia.)

Waambie wanafunzi kufungua sehemu iliyoandikwa barua. Waambie kuwa wajifikirie kuwa katika kanisa la Filipi na Paulo amewaandikia wao barua hiyo. Waambie waandike majina yao katika nafasi iliyoachwa hapo juu.

Someni pamoja barua hiyo. Waambie wataje baadhi ya mambo ambayo Wakristo wa kanisa hilo walikuwa wakitenda yaliyodhuru kanisa lote. (Toa majibu katika barua hiyo.)

Litazame swali hili, "Je, umewahi kuwa hivyo?"

Waambie wanafunzi kufungua katika sehemu ya KAZI YA KUFANYA ya somo hili na wajibu maswali ya Paulo. (Wape muda wa kuandika majibu yao.)

KAZI YA KUFANYA

Ilangalie tena ile barua uliyofikiria kuwa wewe u mmoja kati ya washiriki wa kanisa la Filipi na uliyasikia maneno ya Paulo. Andika jibu la swali uliloulizwa na Paulo katika mwisho wa barua yake kwako.

Kamilisha sentensi hizi kwa usemi uliosahihi.

1. Nikiyasahau a. yaliyo nyuma
2. Nikiyachuchu- milia b. ulifikie lengo.
3. Kaza mwendo c. Katika Kristo Yesu.
4. Mwito mkuu d. yaliyo mbele. wa Mungu

Je, ni watu gani walio kusaidia kukua kama Mkristo? Andika majina ya watu walio kusaidia kukua katika mifano hiyo ya kukatia nguo. Andika sentensi moja ielezayo yale uliyojifunza kutoka kwao.

Uliza: Unafikiri Paulo alitaka waamini waigeje matendo yake? (Wawe waaminifu, watifu, wawe na nia nzuri kuhusu kufaulu na kushindwa, wawe na lengo lifaalo maishani.)

Uliza: Unaweza kuwakumbuka watu ambao wamekusaidia kiroho? (Ngojea majibu.)

Sema: Kila mmoja wetu anaye mtu ambaye amemsaidia kukua kiroho. Anaweza kuwa mchungaji, rafiki yako, au mtu mliyekutana katika mkutano wa Kikristo au wazazi wako. Hebu fikiria jinsi mtu huyo alivyokusaidia. Andika jina lake, au majina ya watu waliokusaidia jinsi ulivyoagiwa katika somo lako. Mtindo ni kama mwongozo. Andika jinsi walivyo-kuongoza katika tabia na nia yako.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wafilipi 3:20-21.

Uliza: Je, inamaanisha nini kusema “wenyeji wetu uko mbinguni?” (Wenyeji unamaanisha uraia, au makao. Uraia na makao ya Mkristo ni mbinguni.)

Uliza: Je, nyumbani kwako ni wapi? Kama wewe u mwamini, kwako ni mbinguni, kama hujaamini, huenda ukachagua mbinguni kuwa nyumbani kwako.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Nakaza mwendo, niifikirie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu” (Wafilipi 3:14).

Wahimiza wanafunzi hao kuandika lengo lao kama Wakristo. Waambie mambo wawezayo kufanya ili walifikie lengo lao. Wasaidie kuandika jambo moja ambalo watafanya wiki hii ambalo litawasaidia kufikia lengo lao.

WAKATI WA MWISHO

Andikeni pamoja sala ambalo wanafunzi hao watatumia pamoja na Mkristo anayekua kiroho. Laweza kuwa na mambo haya:

Mungu Mpendwa,

Asante kwa kunionyesha kwamba nahitaji kukua kiroho. Nisaidie kutokumbuka yaliyopita, ila nikaze mwendo na kufikiria jinsi niwezavyo kukufurahisha. Sitaki kuwapendeza tu wanadamu. Nisaidie kukua niendeleapo kukujua na niwa-ambapo wengine ujumbe wako.

Amina.

Imbeni pamoja wimbo usemao “Nataka Nimjue Yesu”.

Funga kwa maombi.

JE! NANI ANAYENIMILIKI?

MASOMO YA BIBLIA: I Wakorintho 6:9-20

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Unapaswa kujitayarisha vya kutosha ili uweze kufundisha ikupasavyo. Hakikisha kwamba unayaelewa Maandiko. Halafu wafikirie wanafunzi wako. Je, ukweli wa maandiko haya ni wa muhimu kwao? Unawezaje kuwasaidia ili waelewe ukweli huu?

Soma maandiko ya Biblia, halafu usome maelezo yaliyoko katika vitabu vya wanafunzi. Paulo aliwaandikia maneno haya Wakristo wa Korintho. Korintho ulikuwa mojawapo wa miji iliyojaa maovu mengi. Watu wengi waliabudu sanamu. Ibada hii ilikuwa hasa ya kuufanyia mwili maovu. Kuna wakati ambapo zaidi ya malaya elfu moja walitumikia hekalu la ibada hii. Wakristo walioishi Korintho walichanganyikiwa kuhusu utumiaji mwema wa miili yao. Paulo alijua kwamba ni lazima awaeleze wazi kuwa miili yao ni mali ya Mungu. Aliwafundisha kwamba Mungu wa kweli anawataka wafuasi wake kuwa watakatifu kimwili. Paulo anaeleza sababu nne za kuwa watakatifu kimwili katika I Wakorintho 6:9-20. Rudieni sababu hizi zilizoелеzwa katika ukurasa ya wanafunzi.

Wafikirie wanafunzi wako. Unapaswa kufikiria na kuombea matatizo ya wanafunzi wako. Je, wanaelewa walumbwa na Mungu nao ni mali yake? Je, wanajaribi waje kutumia vibaya miili yao? Kama

wanafunzi wako ni wa darasa la nne au la tano hutapaswa kuisisitiza usafi wa uasherati. Hata hivyo, kama ni vijana wakubwa, utapaswa kuzungumzia juu ya nia ya Kikristo kuhusu kufanya mapenzi. Wazazi wengi hawaongei kuhusu jambo hili. Kanisa linajukumu la kufundisha kanuni za Mungu. Wanafunzi wako wanapaswa kufahamu kwamba kufanya mapenzi si kubaya, bali ni karama ya Mungu. Ni lazima waelewe kwamba karama hii inaweza kutumiwa vibaya. Wanapaswa kuelewa kwamba kutokuwa wasafi kimwili ni kutomheshimu Mungu.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi kujua sababu ya kumtukiza Mungu katika miili yao na kuelewa jinsi ya kufanya hivyo.

KULIFUNDISHA SOMO

Waambie baadhi ya wanafunzi utaja sehemu za mwili na jinsi wawezavyo kuzitumia. (Kwa mfano: "Hii ni mikono yangu. Naitumia niendapo kulima.")

Uliza: Je, uko huru kutumia mwili wako jinsi utakavyo? (Ngojia majibu.) Kama ni "la", uliza, ni kwa nini?

Sema: Hatuko huru kutumia miili yetu jinsi tutakavyo kwa sababu tu mali ya Mungu. Ndiye aliyetuumba.

Uliza: Je, mwanadamu amekuwa akiishi kama yeye ni Mali ya Mungu? Ndiye aliyetuumba.

Uliza: Je, mwanadamu amekuwa akiishi kama yeye ni Mali ya Mungu? Je, amemtii Mungu kila mara?

Sema: Biblia inatuambia kwamba mwanadamu alimwasi Mungu. Aliamua kutenda dhambi. Hakuishi kama mwana wa Mungu. Sisi wote tu kama watu wa kwanza walioumbwa na Mungu. Tumekataa kumtii Mungu. Lakini Mungu alitupenda sana hata akamtuma Yesu Kristo ulimwenguni ili kutuonyesha njia ya kumrudia Mungu. Yesu alikufa msalabani ili kulipa deni la dhambi zetu. Alifia kila mmoja wetu.

Tumenunuliwa kwa thamani, yaani damu ya Yesu. Sisi ni mali ya Mungu kwa sababu alituumba na akatuokoa. Kwa hivyo hatuko huru kutumia miili yetu kwa kutenda yale ambayo hayamtukuzi Mungu.

Waambie wanafunzi hao wafungue Biblia zao katika I Wakorintho 6:9-20.

Uliza: Twawezaje kumtukiza Mungu katika miili yetu? (Eleza kuwa "kutukiza" inamaanisha kutenda yale yampendezayo Mungu na yale yatakayolitea jina lake sifa.) Andika majibu yao ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Wanaweza kusema ni kuwa mwana michezo mzuri, kula chakula kifaacho na kumpumzika vya kutosha. Waambie wataje vile vitu viwezavyo kudhuru miili yao na kutomtukuza Mungu. Majibu yaweza kuwa kunywa pombe na kuvuta sigara, kutokula vizuri, uasherati na uzinzi.

Sema: Somo letu la leo latupa mwongozo jinsi ya kuitumia miili yetu.

Sema: Baadhi ya Wakristo wa Korintho walikuwa na shinda. Hawakuwa wamefundishwa kuhusu sheria za Mungu walipokuwa wadogo. Hawakuwa wanajua sheria isemayo, "Usizini." Walikulia katika sehemu

ambayo watu waliabudu sanamu badala ya Mungu wa kweli. Walitumia miili yao kwa kutenda maovu katika ibada waliyofanya. Ilikuwa vigumu sana kwa mwamini (Mkristo) mpya kuacha ibada kama hiyo na kuishi kulingana na amri ya Mungu. Kwa hivyo, Paulo aliwaandikia Wakristo wa Korintho maongozi fulani. Hebu na tusome maongozi haya katika I Wakorintho 6:9-24.

Mhimize kila mwanafunzi kufuata maandiko katika Biblia yake yanaposomwa. Jadili na kueleza maana ya maneno magumu.

Sema: Paulo aliwapa Wakristo maagizo ya kufuata, lakini alisaidia zaidi ya hapo. Aliwatolea sababu za kuwaambia wafuate maagizo hayo. Sababu hizi zinatufaa hata sisi. Hebu tuangalie katika Biblia zetu sababu nne zilizomfanya Paulo kuwaagiza Wakristo kuitunza miili yao.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome kifungu cha 15 hadi 17.

Sema: Unapokuwa Mkristo huwa umeunganishwa na Kristo. Hii inamaanisha kwamba utu wote umeunganishwa naye - mwili na Roho. Roho haiwezi kutenganishwa na mwili unapoishi. Si rahisi kusema, "Nitamtukuza Mungu kwa Roho yangu, lakini si kwa mwili wangu." Haupaswi kutumia mwili wako kwa njia ambayo haitamtukuza Mungu. (Hili ni jambo gumu kwa vijana kuelewa. Utapaswa kulieleza kikamilifu. Hasa, jambo muhimu ni kwamba kila sehemu ya Mkristo - dhamira (akili), mwili na roho, vyapaswa kumtukiza Mungu. Kama

mtu ni mali ya Mungu, basi, mwili wake ni mali ya Mungu pia. Hakuna awezaye kufanya maovu na mwili wake bila kudhuru uhusiano wake na Mungu.)

Mwambie mwanafunzi mwingine asome kifungu cha 18.

Sema: Kifungu hiki kinatuambia sababu ya pili ya kuitunza miili yetu. Paulo anasema kwamba uasherati na zinaa ni dhambi itendayo juu ya mwili. (Uasherati ni ngono baina ya wale ambao hawajaoana. Uzinzi ni ngono baina ya mmoja ya wale waliooana na mtu mwingine.) Paulo alisema kwamba Mkristo hapaswi kufanya ngono na mtu mwingine isipokuwa yule aliye hwoa. Alielekeza maagizo yake juu ya mpango wa Mungu jinsi ulivyoelezwa katika kitabu cha Mwanzo. Ngono si mbaya, bali ni karama ya Mungu. Mungu aliitoa karama hii ili wale waliooana waweze kupata watoto na kuonyeshana upendo wao. Wakristo hawapaswi kutumia vibaya karama hii kwa sababu wao ni mali ya Kristo. (Mwalimu yale utakayoongea kuhusu somo hili yatategemea umri wa wanafunzi na uwezo wao wa kuelewa. Kumbuka kwamba ni rahisi kwao kusikia mafundisho ya Kikristo kuhusu kufanya mapenzi, kuliko kusikia mafunzo mabaya kutoka kwa wale wasio Wakristo.)

Mwambie mwanafunzi mwingine asome kifungu cha 19.

Sema: Hiki ndicho kifungu chetu cha kukumbuka. Tunamaanisha nini tunaposema kwamba mwili ni hekalu la Roho Mtakatifu? (Ngojea majibu.)

Ukiisha itikia majibu yao, sema hivi: Mnakumbuka kwamba Wayahudi waliabudu katika "hekalu". Hekalu la Yerusalemu lilijazwa na utukufu wa Mungu lilipotolewa wakfu kwake. Unapokuwa Mkristo, huwa unasema kwamba, "Kristo, nakutaka uishi ndani yangu. Kwani najitoa wakfu kwako." Wakati huo huo Kristo huanza kuishi ndani yako katika Roho wake Mtakatifu. Huwa sawa "hekalu" au "nyumba" ya Roho Mtakatifu. Mwili wako huwa mali ya Kristo. Haupaswi sasa kutumia mwili wako kwa kutenda maovu bali kwa kumtukuza Mungu. Kwa hivyo, sababu ya tatu ya kuutunza mwili wako ni kuwa u hekalu la Roho wa Mungu.

Mwambie mwanafunzi mwingine asome 1 Wakorintho 6:19b-20.

Sema: Tunapata sababu ya nne ya kuitunza miili yetu katika vifungu hivi. Paulo aliwakumbusha Wakorintho kwamba Kristo alikuwa amewalipa deni la wokovu.

Uliza: Ni nani aliye kufa msalabani kwa ajili yako? (Yesu)

Sema: Wewe ni mali ya Kristo kwa sababu alikufa msalabani kwa ajili yako. Amekununua na damu yake. Mwili wako si mali yako ya kufanyia cho chote utakacho. Unapaswa kuutumia mwili wako kwa utukufu wa Kristo, wala si kwa kutimiza tamaa.

Sema: Tumesoma na kujifunza sababu nne muhimu, ambazo Biblia inatueleza jinsi tuwezavyo kumtukuza Mungu kwa miili yetu. Sasa hebu tufikirie jinsi tuwezavyo kutii maagizo haya. (Schemu ya KAZI YA KUFANYA ya somo hili ndiyo

itakayowasaidia wanafunzi kuelewa jinsi ya kutumia ukweli ulioeleza maishani mwao. Unapaswa kuwahimiza zaidi kuliko kuwaambia tu wajibu maswali. Wasaidie kuelewa maana ya ukweli huu maishani mwao. Majibu hayajatolewa katika sehemu ya kwanza kwa sababu hii inategemea jibu la kila mwanafunzi.)

KAZI YA KUFANYA

Yohana ni Mkristo. Anajua kwamba anapaswa kufuata maagizo ya Mungu kwa kuutunza mwili wake. Soma sentensi zifuatazo. Zinatuambia baadhi ya njia ambazo Yohana hutumia mwili wake kwa kumtukuza Mungu. Weka alama ya (✓) kando ya yale ambayo nawe unatenda, na uweke alama ya (X) kando ya yale ambayo hufanyi, lakini ungetaka nawe uanze kuyafanya.

- Yohana hula chakula kizuri na hufanya mazoezi na kuwa na wakati wa kupumzika.
- Hukataa kutumia lugha au maneno mabaya wakati wenzake wafanyapo hivyo.
- Wakati wenzake waanzapo kusema hadithi zisizofaa (chafu), yeye huondoka mahali hapo.
- Rafiki yake mmoja alijaribu kumhimiza anywe pombe ili ajisikie kuwa “mtu mzima”, lakini yeye alikataa kufanya hivyo. Alimweleza kwamba pombe si nzuri kwa mwili wake Pia, alimwambia rafiki yake huyo kwamba akikubali kunywa wakati huo, basi itakuwa vigumu kwake kukataa kunywa wakati mwingine.

Soma 1 Wakorintho 6:15-20. Baada ya kusoma vifungu hivi, soma maelezo yafuatayo, yanayoeleza maana yake. Jaza nafasi iliyoachwa kwa kutumia maneno yaliyo sahihi.

Je, hujui kwamba yale ufanyayo kama Mkristo humhusu Kristo? Biblia inatuambia kwamba hiyo ni kweli. Tuwapo Wakristo huwa ni sehemu ya MWILI ya Kristo. Tunapo ufanyia mwili wetu maovu, huwa tunam-sitikisha KRISTO na sisi wenyewe pia.

Paulo aliwakumbusha 1 WAKORINTHO kwamba wanapaswa kujihadhari na dhambi ya zinaa. Aliwaeleza kwamba wanapotenda dhambi hii huwa hawasahau tu thamani ya miili yao, bali hata thamani ya wenzao. PAULO aliwaonya kwamba wanapaswa kuikimbia zinaa. Aliwakumbusha kwamba wanapaswa kuutumia mwili na roho zao kwa kumtukuza MUNGU.

Soma tena vifungu vilivyo-orodheshwa hapo chini na uandike sababu za kuutunza na kuulinda mwili wako.

Pengine unautumia mwili wako kwa njia ambayo haimtukuzi Kristo. Huenda ikawa umezoea jambo hilo na hujui jinsi ya kuliacha. Hebu mwangalie kijana aliyoko katika picha hii. Amenaswa katika utando wa buibui na hawezi kamwe kujiokoa. Je, wewe u kama kijana huyu? Je, umenaswa na tabia mbaya kama utando? Biblia inatuambia kwamba Mungu ana uwezo wote. Anaweza kukusaidia kuishinda tabia mbaya. Sasa mwombe ili akujaze na uwezo utakao kusaidia kuacha



kutenda yale ambayo yanakuzuia kumtukuza Mungu kwa mwili wako.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu?” (1 Wakorintho 6:19).

Waongoze wanafunzi wako katika kusema pamoja kifungu cha kukumbuka. Waweza sasa kumsikiliza au kuandika jina la kila mmoja asemapo kifungu hiki. Wape wanafunzi hao muda wa kujibu maswali yahasuyo kifungu cha kukumbuka. Waelezee tena maana ya kifungu hicho.

WAKATI WA MWISHO

Uliza: Je, kichwa cha somo hili ni kipi?

Uliza: Je, unaweza kutoa sababu ufikiriazo kwamba wewe ni mali ya Mungu? (Waongoze wanafunzi hao kukumbuka kwamba miili yetu iliumbwa na Mungu, wamenunuliwa kwa thamani na Kristo, nao wameunganishwa naye, na kwamba Roho Mtakatifu huishi ndani ya kila Mkristo.

Wakumbushe wanafunzi hao kwamba Mungu hujali miili ya watu. Huwatimizia mahitaji yao ya kimwili jinsi aliwaponya wagonjwa na kuwalisha watu elfu tano.

Uliza: Je, mnamajibu ya kuongezea swali nililouliza mwanzoni wa somo hili? Je, mmefikiria jinsi mwezavyo kumtukuza Mungu kwa miili yenu? (Ongezea orodha ya majibu uliyoandika hapo awali).

Malizia kwa kumwomba kila mmoja ili amtukuze Mungu kwa mwili wake aliopewa naye.

SURA YA NANE

UHURU NA WAJIBU

MASOMO YA BIBLIA: I Wakorintho
10:23-11:1

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! wewe hufanya nini unapojiandaa kufundisha? Unapaswa kuanza mapema kuyasoma Maandiko ya Biblia uliyopewa. Soma somo lote katika kitabu cha mwalimu na cha wanafunzi. Wafikirie wanafunzi wako unapo soma somo hilo. Je! unajua mahitaji yao? Umewahi kuwatembelea nyumbani kwao? Je, huwa unamwomba kila mmoja?

Ni lazima mwalimu mzuri azoe kujifunza, anapaswa pia kufanya zaidi ya hapo. Ni lazima awafahamu wanafunzi wake na hasa ayajali maisha yao. Ni lazima ategemea uongozi wa Rôho Mtakatifu anapoyaeleza maandiko na jinsi yanavyohusu maisha ya wanafunzi hao.

Somo hili litawasaidia kutambua kwamba wanapaswa kufikiria jinsi matendo yao yawahusavyo wenzao. Watoto wakubwa na vijana wanaanza kufahamu kwamba wao ni watu tofauti na wazazi wao. Wanafahamu kwamba ni lazima wafanye uamuzi wao wenyewe bila kuambiwa na jamaa zao. Wao hupenda kusema kwamba, "Haya ni maisha yangu nami nitaishi jinsi nitakavyo." Unaweza kuwasaidia ili watambue kwamba kuwa huru hakumaanishi kufanya jinsi utakavyo.

Maandiko ya Biblia yatawasaidia wanafunzi hao kuelewa kwamba tabia za Wakristo zaweza kusaidia au

kumzuia mtu mwingine kutomjua Kristo. Au, yanaweza kuzuia au kumsaidia Mkristo kukua kiroho.

Wanafunzi wako watazidi kutambua kwamba ni muhimu kuwa na utu wema na kuwa msikivu. Hizi ndizo ishara za Mkristo akuaye.

Soma I Wakorintho 10:23 hadi 11:1. Sasa soma maelezo ya vifungu hivi yaliyoko katika kitabu cha wanafunzi. Utatakiwa kuwa tayari kuwasaidia wanafunzi wako ili waelewe jinsi ya kutumia wajibu wa uhuru wao. Mawazo haya ya Paulo kuhusu kula nyama na matendo yake kwa wenzake yatakusaidia sana. Wasaidie wanafunzi wako kutambua kwamba huwa na jukumu wanapoamua kuacha tabia fulani kwa ajili ya kazi ya Mungu.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi kutaja sehemu ya maisha yao ambayo wangependa kuwekea uhuru wao kiwango fulani kwa ajili ya wenzao.*

KUFUNDISHA SOMO

Waambie wanafunzi wawili "kuiga" majadiliano baina ya Yohana na Yusufu ambayo ndiyo mwanzo wa somo lao. Waambie kwamba wanaweza kusoma au kusema tu.

Uliza: Ungejibuje swali la Yohana? Je, Mkristo anaweza kuishi tu bila kufikiria jinsi anavyowahusu watu wengine? (Wape muda wa kujadiliana kabla ya kujibu.)

Soma maandiko ya Biblia. Andika usemi ufuatao ubaoni au kwenye karatasi: “Wakristo wanao wajali wenzao wataweka kiwango cha uhuru wao kwa ajili ya wenzao.”

Uliza: Je, usemi huu una maana gani kwako? (Jadiliana)

Sema: Leo, tutajifunza yale ambayo Paulo aliwaambia Wakristo wa Korintho miaka mingi iliyopita kuhusu uhuru na wajibu.

Sema: Wakristo wa Korintho walikuwa wamemwandikia Paulo kuhusu shida iliyokuwepo kanisani mwao. Walitaka kujua ikiwa Mkristo anastahili kula nyama iliyotolewa kama dhabihu kwa miungu. Wanyama wengi walichinjwa katika hekalu la wasio Wakristo. Sehemu ya nyama hiyo iliteketezwa madhabahuni, na nyingine ikapatiwa makuhani wao. Iliyobakia ilipelekwa na kuuzwa sokoni. Kulingana na Wakorintho nyama hiyo ilikuwa “imebarikiwa” na kuhani aabuduye sanamu. Je, Mkristo anastahili kuinunua na kuila? Au ulaji wa nyama hiyo waweza kumdhuru Mkristo dhaifu au yule asiye Mkristo?

Waambie wanafunzi hao wafungue Biblia zao katika 1 Wakorintho 10:23. Gawa wanafunzi hao katika makundi matano. Patia kila kundi vifungu vifuatavyo na uwaambie watafute yale visemayo kuhusu wajibu wa tabia ya Mkristo. Kazi hii inaweza kupewa kila mmoja ikiwa wanafunzi hao hawawezi kutoshea makundi matano.

Kundi la kwanza: 1 Wakorintho 10:23-24

Kundi la pili: 1 Wakorintho 10:25-26

Kundi la tatu: 1 Wakorintho 10:27-30

Kundi la nne: 1 Wakorintho 10:31-33

Kundi la tanò: 1 Wakorintho 11:1

Lipe kundi la kwanza muda wa kueleza yale walioyapata kuhusu wajibu wa tabia ya Mkristo. Vifungu hivi vinatuambia kwamba VITU VYOTE NI HALALI, LAKINI VYOTE HAVIFAI WALA KUTU-SAIDIA KIROHO.

Sema: Paulo alikuwa akisema kwamba Mkristo anaweza kufanya jambo lo lote ambalo si la dhambi kwake. Hata hivyo, aliongezea kwamba yeye anapaswa kuwa na kiwango cha uhuru wake kwa ajili ya wenzake. Alijua kwamba sanamu haimaanishi cho chote. Iliwakilisha kitu ambacho hakipo kabisa. Kwa hivyo, nyama hiyo haikuwa na madhara yo yote kwa sababu sanamu halikumaanisha cho chote. Baadhi ya Wakristo walikuwa na shida ya kuelewa jambo hili. Walifikiria kwamba Mkristo hapaswi kuhusika na kitu cho chote kihusucho ibada ya sanamu. Paulo alikuwa akiwafikiria Wakristo alipoandika maneno haya, “kwa hiyo, chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu” (1 Wakorintho 8:13). Paulo hakuona kosa lolote katika kula nyama hiyo. Lakini alikataa kuila ilipomletea shida mtu mwingine.

Liambie kundi la pili kutoa maelezo yao. Vifungu hivi vinasema kwamba KILA KITU KILICHOKO DUNIANI NI MALI YA BWANA. Wakristo wa

Korintho hawakupaswa kuuliza maswali kuhusu nyama iuzwayo sokoni. Wao wangeinunua na kuila.

Sasa ni wakati wa kundi la tatu. Vifungu hivi vinatuambia kwamba mtu anapaswa kula chakula bila kuuliza swali lo lote iwapo ataalikwa nyumbani kwa asiye Mkristo. Lakini hapaswi kukila iwapo mgeni huyo atamjulisha kwamba chakula hicho kimetolewa dhabihu kwa sanamu. Pengine mgeni mwenzake si mwamini lakini anafikiri sio vizuri kwa Mkristo kula nyama kama hiyo. Au anaweza kuwa Mkristo aliyeona kwamba sio vizuri kula nyama kama hiyo. PAULO ALISEMA KWAMBA HATAKULA NYAMA KWA SABABU YA UPENDO NA KUJALI MGENI MWENZAKE. Angeacha kula nyama hiyo kuliko kumkwaza Mkristo mwenzake au yule anayenuia kuwa Mkristo.

Kundi la nne lapaswa kueleza kwamba tunapaswa KUFANYA JAMBO LO LOTE KWA UTUKUFU WA MUNGU. Usiwakwaze wenzake. Fanya yale yawezayo kuwaelekeza wenzako kupata wokovu katika Kristo.

Kundi la tano lapaswa kusema kwamba kifungu chao kinaeleza yafuatayo: Paulo angewaambia Wakorintho wamfuata kwa sababu alikuwa akimfuata Kristo. TUNAPASWA KUMFUATA KRISTO. TUNaweza 'KUWAHIMIZA WENGINE NAO WAMFUATE, IWAPO TUTAMFUATA.

Kila kundi limeeleza kanuni ya kibiblia ambayo ni mwongozo kwetu tunaponuia kufanya uamuzi. Jadili jinsi kanuni hizi zinavyohusu maisha ya


wanafunzi hao. Waweza kuwauliza maswali haya. Hawapaswi kuyajibu bali kuyafikiria tu.


1. Je! Ulisaidiwa na matendo ya mtu mwingine ulipoamua kuwa Mkristo?
2. Je! Matendo ya mtu mwingine yalikuzuia kutokuwa Mkristo mapema?
3. Je! Usemi huu una makosa gani, "Naweza kufanya jinsi nitakavyo"?

(Sisitiza kwamba tuko huru kutenda yale yampendezayo tu Mungu na pia nilazima tuwe na kiwango iwapo uhuru wetu utamkwaza mtu mwingine.)

KAZI YA KUFANYA

Waambie wanafunzi hao wafikirie jinsi walivyo huru na wajibu walio nao. Sasa waambie wajaze nafasi iliyoachwa katika sentensi zilizoko kwenye vipepeo vifuatavyo. Jadiliana majibu yao.





kuyatenda, lakini yanaweza kuwadhuru sana wenzao. Wahimize ili wayaandike na waamue hatua watakayoyachukulia. Somo letu la leo litawasaidia kuwa na kiwango cha uhuru wao kwa ajili ya wenzao.

Waambie wainamishe vichwa vyao na wamwambie Mungu uamuzi waliofanya. Sasa ongoza kwa maombi yatakayomwezesha kila mmoja kuwa na kiwango katika mambo aliyoandika.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi” (1 Wakorintho 9:19).

Wape wanafunzi wako muda wa kusema kifungu cha kukumbuka. Unaweza kujiwekea orodha jinsi kila mmoja anavyokariri. Jambo hili litawahimiza wanafunzi hao kukariri vifungu hivyo kila wiki.

Sema: Paulo alikuwa mtumwa wa dhambi, lakini alifanywa huru na Yesu Kristo. Alikuwa mtumwa wa sheria, lakini Kristo alimfanya kuwa huru. Unaweza kufikiria kwamba Paulo angetumia uhuru huu alionao kufanya jinsi atakavyo. Haikuwa hivyo kamwe. Alitambua kwamba ni lazima awe na kiwango cha uhuru huo ili awavute wengine wamjue Kristo. Alisema kwamba yeye alijifanya mtumwa wa wote.

Ongoza wanafunzi kuwaza juu ya maisha yao. Waruhusu waandike vitabuni mwao mambo matatu wanayodhania kuwa ni mema kwao

JAMAA YA KIKRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Waefeso 5:21-25; 6:1-4

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Bila shaka umetambua kwamba si rahisi kufundisha masomo ya miezi hii jinsi ilivyokuwa kwa masomo ya kwanza. Hasa hauna hadithi ya Biblia ambayo utawasimulia watoto. Pengine itakuwa vigumu kujua jinsi utakavyoeleza Maandiko haya kulingana na maisha ya wanafunzi hao. Hii inamaanisha kwamba utatakiwa kutumia muda mwingi kwa kujiandaa kikamilifu. Hata ingawa masomo haya ni magumu, ni ya muhimu sana kwa wanafunzi wako. Hebu fikiria nyumbani watokako. Je! Wana mahitaji yapi?

Uhusiano baina ya jamaa na vijana huzusha matatizo mengi. Wao hushughulika sana ili waelewane na wazazi wao, ndugu na dada zao. Mara nyingi uchoyo huwa ndicho chanzo cha matatizo haya. Kijana huwaza tu yale anayotaka. Hujifikiria kuwa hana muda wa kufikiria mahitaji ya wenzake. Wazazi wanaweza kuwa na kazi nyingi hata wasipate muda wa kuwa na watoto wao.

Hitaji lingine la vijana ni kutaka kujua jinsi ya kutii. Mara kwa mara huwa hawaoni thamani ya kuwa watiifu. Wakuu wao wanaweza kuwa wazazi. waalimu au waalimu wakuu. Wanaweza kuwafikiria watu hao kuwa ni "wazee" ambao hawajui mambo ya siku hizi. Vijana walio wakubwa zaidi hujaribu kujipatia uhuru. Wafanyapo

hivi huanzisha migongano baina yao na wakuu wao. Somo hili litawasaidia wanafunzi wako kujua maana ya kujitoa au kutii. Watatambua kwamba nyumba ya Wakristo inapaswa kuwa na ushirika mwema baina ya wazazi na watoto na pia mume na mke wanapaswa kuheshimiana. Wanapaswa kuelewa kwamba uhusiano huu huwepo wakati mtu anapojitoka kabisa kwa Kristo.

Soma vifungu hivyo vya Waefeso. Sasa soma somo lililoko katika kitabu cha wanafunzi. Maelezo haya yatakusaidia kuyaelewa maandiko ya somo hili.

Kusudi la somo hili ni kuwaongoza wanafunzi ili waelewe jinsi kujitoka kwao kwa Kristo kwaweza kudhihirishwa katika uhusiano wao na jamaa zao.

KULIFUNDISHA SOMO

Anza kwa kuwasomea yafuatayo. Pengine ni hadithi tu, au pengine ni ya kweli. Waongoze wanafunzi katika kufikiria juu ya habari hiyo. Wataapaswa kutoa madokezo ya kutatua tatizo hili.

Maria alikuwa na jukumu la kazi aliyopewa shuleni mara tu aliporudi nyumbani kila jioni. Siku moja hakumaliza kazi yake kwa sababu aliitwa na rafiki zake ili waende kucheza pamoja. Mamake aliporudi kutoka shambani, alimwuliza kama amemaliza kazi yake ya shule. Maria aliogopa kumwambia ukweli, asije akapatwa na shida. Maria anapaswa afanyeje?

Wape muda wa kujadiliana kuhusu habari uliyowasomea na wadokeze jinsi wawezavyo kujibu swali hili, "Maria anapaswa afanyeje?" Uliza: Je, ukristo wa Maria utahusu yale atendayo?

Uliza: Je, unapokosana na wazazi wako, huwa unasema, "Nitabadilika sana niwapo mzazi?" Waeleze kwamba somo la leo litatusaidia kuelewa jinsi mume na mke wanavyopaswa kushirikiana. Pia, litatusaidia kuelewa jinsi watoto wapaswavyo kushirikiana na wazazi wao.

Uhusiano kati ya jamaa umekuwa chanzo cha matatizo mengi sana. Hapakuwa na tofauti yo yote wakati wa Paulo. Paulo alionelea kwamba yafaa imani ya Mkristo ilete tofauti baina ya uhusiano wa wazazi na watoto, pia kati ya uhusiano wa mume na mke.

Sema: Paulo alitoa mwongozo wa kuwasaidia Wakristo kujua jinsi ya kuishi kama jamaa. Mwongozo huu unaweza kutusaidia hata na sisi.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waefeso 5:21. Sema: Mwongozo huu unawahusu Wakristo wote. Nao ni upi? (Ngojea majibu.) Ndiyo, Wakristo wanapaswa kunyenyekeana. Je! unajua maana ya "kuwa mnyenyekevu?" (Ikiwa hakuna jibu kamili, sema maelezo haya.) Sema: 'Kunyenyekea' inamaanisha kuwashughulikia wenzako kabla ya kujifikiria wewe mwenyewe. Paulo alisema kwamba Wakristo wanapaswa kunyenyekeana kwa sababu wanampenda na kumtii Kristo.

Mwambie mwanafunzi mwingine asome Waefeso 5:22-26. Waambie nusu ya wanafunzi hao kusikiza yale mume

apaswayo kufanya, na ile nusu nyingine isikilize yale yapaswayo kutendwa na wake. Waambie wanafunzi hao waeleze yale waliyosikia baada ya kumaliza kusoma.

Sema: Paulo aliwaambia wake kuwatii waume zao. Hawakuwa akiwaambia wake tu, bali alikuwa akiwaambia hata waume. Kila mmoja hapaswi kutenda jinsi atakavyo, bali anapaswa kufikiria mahitaji ya mwenzake kwanza. Mke Mkristo anapaswa kumheshimu mumewe. (Soma maelezo zaidi katika kitabu cha mwanafunzi.)

Uliza: Mmesikia kwamba waume wanapaswa kufanyeje? (Ngojea majibu) Sema: Ndiyo, waume wanapaswa kujitoa kwa ajili ya wake zao. Paulo aliwaambia kwamba wanapaswa kuwapenda wake zao jinsi Kristo apendavyo kanisa. Je, Kristo alilipendaje kanisa? Ndiyo, alilipenda sana hata akafa kwa ajili yake.

Sema: Pengine unashangaa kwa nini ni muhimu kwangu kujua habari hii? Kwa kweli, unapaswa kuanza sasa kujitayarisha kwa ajili ya ndoa ya Kikristo. Utafanya hivyo kwa kujua tu mwongozo wa Mungu kwa waume na wake.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waefeso 6:1-4. Sasa waambie wanafunzi wasikilize maagizo wapewayo watoto. Waambie sasa kufungua katika sehemu yao ya KAZI YA KUFANYA na waandike maagizo haya katika picha ya mshale wa kwanza. Wanaweza kuwa wameisha jaza nafasi hiyo Kama wamemaliza,

watatakiwa kusoma tena maagizo hayo.

Mwambie mwanafunzi mwingine asome tena vifungu hivyo. Wakati huu waambie wale wengine kusikiliza maagizo yatolewayo kwa wazazi. Waambie waandike maagizo haya katika picha ya mshale wa pili.

Sema: Watoto wameagizwa kuwatii wazazi wao kwa sababu hivyo ndivyo Mungu alivyowataka wafanye. Wale wanaotii wazazi wao wataishi kwa furaha kuliko wale ambao hawatii. (Jadili kuhusu shida yo yote ambayo watoto wanaweza kuwa nayo kwa kuwatii wazazi wao. Wasaidie kuelewa kwamba kila mmoja yuko chini ya mamlaka ya mtu fulani.)

Sema: Paulo aliwaandikia wazazi kifungu cha mwisho cha somo hili. Aliwaambia kwamba hawapaswi kuwachokoza watoto wao. Hii inamaanisha kwamba hawapaswi kuwakaripia wala kuwagombeza watoto wao. Tabia kama hii huwafanya watoto kukasirika haraka na kukosa adabu nzuri. Pia, aliwaambia wazazi kwamba wanao wajibu mkuu wa kuwafundisha watoto wao jinsi ya kuishi kama Wakristo. Kuwa mzazi si jambo rahisi. Lakini unaweza kuwasaidia wazazi wako kwa kuwa mtiifu.

KAZI YA KUFANYA

Wasaidie watoto kumalizia sehemu yao ya KAZI YA KUFANYA kama hawajaimaliza. Hakikisha kwamba wanaelewa jinsi ya kujipima. Sisitiza kwamba kama majibu yao ni "la" basi, wangali na mengi ya kujifunza kuhusu utii. Wahimiza waandike jinsi

wawezavyo kujiendeleza. Huu ndio wakati ambao unapaswa kutumia ukweli wa Biblia. Haitoshi kujifunza tu yale yasemwayo na Biblia.

Majibu ya sehemu ya kwanza hayajatolewa kwa sababu kila mwanafunzi anapaswa kujibu mwenyewe. Nakala ifuatayo iko katika kitabu cha wanafunzi.

Vifungu hivi ulivyosoma katika Waefeso vina maagizo ya kuisaidia jamaa ya Kikristo kuishi pamoja kwa upendo. Maagizo haya ni kwa wake na waume, wazazi na watoto.

Je! Unapokosa kukubaliana na wazazi wako, wewe husema, "Nitabadilika niwapo mzazi?" Angalia maisha yako ya sasa kama unataka kujua aina ya mzazi utakaye kuwa. Hivyo ndivyo utakuwa uwapo mtu mzima. Je! Wewe ni nani?


Jibu kila swali na mojawapo ya maneno yafuatayo: Kila mara, wakati mwingine, hata kidogo:

1. Je, ninawatii wazazi wangu? ____
2. Je, ninatii sheria? ____
3. Je, wazazi wangu wanaweza kuniamini? ____
4. Je, niko tayari kuwasikiliza wazazi wangu? ____
5. Je, mimi ni mchoyo? ____
6. Je, ninawajali wengine? ____
7. Je, niko tayari kukubali ninapokosa? ____

Je, ungependa kurekebisha baadhi ya tabia hizi? Kama unataka, basi andika hapo chini jinsi utakavyojirekebisha.


Soma tena Waefeso 6:1-4. Soma vifungu hivi kimoyomoyo. Andika katika picha ya mshale huu maagizo yaliyotolewa kwa watoto:

W
A
T
O
T
O



Andika maagizo yaliyotolewa kwa akina baba.

W
A
B
A
B
A



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana Mungu wako” (Kutoka 20:12).

Sema: “Kuheshimu” inamaanisha kupenda na kutii. Nyumba ya Wakristo huwa na upendo. Ikiwa unampenda

Yesu, bila shaka utaipenda jamaa yako. Hutakuwa ukikubaliana nao kwa kila jambo. Lakini utawasaidia na kuwaombea.

Sema: Pengine wazazi wako watakutaka ufanye jambo ambalo waona halifai. Hata hutaielewa kwa nini wanakutaka ulifanye. Waweza kuwaza kuwa, “Wazazi wangu wamezeeka. Hawana kisomo kama changu. Hata hawajui mahitaji ya vijana wa siku hizi.”

Ni kweli kwamba nchi yetu inabadilika. Hata pengine wazazi wako hawajui sana mitindo na hali ya siku hizi. Lakini kumbuka kwamba, wao wameishi sana na wana maarifa mengi kuliko ninyi. Wanakupenda na wanakutakia yaliyo mema. Kwa hivyo, watii wazazi wako. Unapaswa kuwajali kuliko nafsi yako mwenyewe. Watii.

Waongoze watoto hao katika kukariri kifungu cha kukumbuka. Tumia mtindo wa wote utakao kuwatambua wale waliojifunza kifungu hicho.

WAKATI WA MWISHO

Rudia hasa mkazo wa somo hili. Tazama katika sehemu ya kusudi la somo hili. Je, umewaongoza wanafunzi kuelewa jinsi kujitoea kwao kwa Kristo kunaweza kudhihirisha uhusiano wao na jamaa yao?

Waambie sasa wajaze nafasi iliyoachwa mwishoni mwa sehemu ya KIFUNGU CHA KUKUMBUKA kama kazi yao ya mwisho. Majibu yake yameandikwa hapo chini.

Kuna baadhi ya vifungu katika Biblia ambavyo vinatuambia jinsi ya kuishi na jamaa zetu. Visome na ujaze nafasi zilizoachwa katika vifungu hivyo.

-Wapenzi, na TUPENDANE...

(1 Yohana 4:7)

-Tena iweni WAFADHILI ninyi kwa ninyi wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika KRISTO alivyowasamehe ninyi.

(Waefeso 4:32)

-Enyi watoto, WATIINI wazazi wetu katika Bwana, maana hii ndiyo haki.

(Waefeso 6:1)

SURA YA KUMI

MSAIDIZI MKUU

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 14:16-17, 25-26; 16:7-15; Wagalatia 5:22-23

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Unapojiandaa kufundisha somo lo lote, unapaswa kuyafikiria mahitaji ya wanafunzi wako. Baadhi yao wanaweza kuwa na shida ya kujizuia, wajaribiwapo. Wengine wanaweza kujisikia pweke au kujiona kama hakuna anayewajali. Watu watahitaji kuelewa vyema ukweli huu wa Biblia. Pia, watatambua kwamba wanahitaji kusaidiwa ili wakue kama Wakristo.

Kusudi lako kama mwalimu ni kuwasaidia wanafunzi hao kuelewa kwamba Roho Mtakatifu yupo. Ni Roho wa Mungu awezaye kuwasaidia katika shida zao na kuwaongoza kuishi maisha yampendezayo. Mungu.

Vifungu vya Biblia vya masomo ya miezi hii mitatu vimeandikwa na Paulo. Pengine leo umeshangaa kwa nini tunatumia vifungu vya Injili ya Yohana na kutoka kwa Wagalatia katika somo la wiki hii. Paulo aliandika mengi kuhusu Roho Mtakatifu na kazi yake maishani mwa Mkristo. Lakini, baadhi ya maandiko yake hayaeleweki kwa urahisi. Mwandishi wa somo hili ametumia maandiko ya Yohana, ili watoto waweze kuelewa vyema Roho Mtakatifu. Maneno ya vifungu hivi ndio yale Yesu aliyowaambia wanafunzi wake. Aliyasema ili kuwaeleza wanafunzi wake kwamba baada ya kurudi kwa Baba yake atawatumia msaidizi. Wewe kama

mwalimu, utafaidika kwa kusoma baadhi ya maandiko ya Paulo. Utapaswa kusoma Warumi 8 pamoja na maandiko uliyopewa hapo juu katika wiki hii.

Unapojiandaa kufundisha utatakiwa kusoma cho chote kiwezacho kukusaidia kuelewa vyema maandiko. Mwambie mchungaji wako au rafiki yako kuwa unahitaji somo lo lote liwezalo kukusaidia. Pengine utaanza kuweka pesa za kuweza kujinunulia kitabu cha kukusaidia katika masomo ya Biblia. Ikiwa utaanza kwa kununua vitabu vichache, basi uendeleapo waweza kuanzisha maktaba ya kusaidia jamii nzima. Kwa sasa, itakubidi usome maelezo ya somo hili yaliyoko katika karatasi ya wanafunzi.

Kusudi la somo hili ni *kuwasaidia wanafunzi wako kumwelewa Roho Mtakatifu na kujua jinsi awezavyo kuwasaidia ili waishi maisha ya Kikristo.*

KULIFUNDISHA SOMO

Waambie wanafunzi wawili kuiga mazungumzo yaliyoko mwanzoni mwa somo hili. Mmoja wao anapaswa awe Yakobo na mwingine awe Mchungaji.

Uliza: Je, wewe hujisikia jinsi Yakobo alivyojisikia? Je, huwa na matatizo ambayo huhitaji kusaidiwa? Je, huwa unawaza kwamba iwapo Yesu angekuwa anaishi hapa duniani ungemwambia akusaidie? (Wape muda wa kujadiliana).

Sema: Tunajua kwamba Yesu alienda mbinguni baada ya kufufuka

katika wafu. Lakini hakutuacha bila msaidizi. Alimtuma Roho Mtakatifu kuenenda pamoja nasi na kuishi ndani yetu.

Uliza: Je, ni habari ipi ujuayo kuhusu Roho Mtakatifu? Tunataka tupate leo majibu ya maswali matatu:

1. Roho Mtakatifu ni nani?
2. Je, yeye hufanya kazi gani?
3. Anawezaje kubadilisha maisha yangu? Ikiwa umesoma somo lako, bila shaka unajua majibu, lakini hebu tuyajadili pamoja. (Andika swali la kwanza ubaoni au kwenye karatasi kubwa.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 14:16-17 na mwingine asome 14:25-26.

Sema: Yesu alipokuwa hapa duniani alikuwa mahali pamoja kwa wakati mmoja. Aliporudi mbinguni alimtuma Roho Mtakatifu ili awe katika kila Mkristo wakati wote.

(Si rahisi kuwaelezea watoto Roho Mtakatifu ni nani. Sisi humfahamu vizuri tunapomruhusu kuishi ndani yetu. Hata hivyo, jaribu kueleza mambo yafuatayo.)

Sema: Roho Mtakatifu ni Mungu. Kuna Mungu mmoja. Amejidhihirisha kwetu kwa namna tatu: Kama Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Je, ni vigumu kuelewa ukweli huu? Hebu ufikirie mfano huu. Mfikirie mama yako. Kwako yeye ni mama mzazi. Naye pia ni mtoto wa wazazi wake. Tena ni mke wa babako. Ingawa yeye ni mtoto, mke na mama, yungali mtu mmoja tu.

Uliza: Je, mfano huu umekusaidia kuelewa? (Wape muda wa kujadiliana.)

Sema: Roho Mtakatifu ni mtu. Ni muhimu kwenu kukumbuka ukweli huu. Katika vifungu tulivyosoma, tunaona kuwa Yesu amemwita Roho Mtakatifu Msaidizi, anayetufunulia ukweli wa Mungu. Hatupaswi kamwe kumfikiria Roho Mtakatifu kuwa kitu tu, lakini kuwa yeye ni mtu.

Andika sasa swali la pili chini ya lile la kwanza. Andika hivi: Je, Roho Mtakatifu hufanya nini?

Uliza: Je, kila mmoja wenu anaweza kuniambia kile afikiriacho kuwa Roho Mtakatifu hufanya? (Ngojea majibu.)

Sema: Hungeweza kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu wakati Yesu alipowaahidi wanafunzi wake kumtuma mtu ambaye angechukua mahali pake. Umesha soma kuwa yeye ni msaidizi na pia mwalimu. Hebu sasa tusome Yohana 16:7-15 ili tuone kama tunaweza kupata maelezo kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 16:7-15. Sema: Vifungu hivi vinatuambia kwamba Roho Mtakatifu huwashawishi wale wasio Wakristo kujua kwamba wao ni wenye dhambi. (Wasimulie hadithi hii na kuwafafanulia maana yake.) Msichana mdogo aliyezaliwa akiwa kipofu alifanyiwa upasuaji wa macho. Siku hiyo daktari alitoa kwa uangalifu gamba lililomzuia kutoona, mtoto huyo aliweza kuona kwa mara ya kwanza! Akasema, "Mama! Mbona hukuni-ambia kuwa kila kitu ni kizuri?"

Sema: Sote huzaliwa tukiwa vipofu kiroho. Hatuwezi kuona yale aliyotufanyia Mungu. Lakini, Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani yetu. Huwa tunaonyesha dhambi zetu na upendo wa Mungu katika Kristo. Huona jinsi Kristo alivyo wa ajabu. Roho Mtakatifu hutusaidia kuona hitaji letu la kupata wokovu. Hutusaidia kujua ukweli kuhusu Yesu Kristo.

Waambie wanafunzi wafungue katika sehemu yao ya KAZI YA KUFANYA na wajaze nafasi iliyoachwa ya swali la kwanza. Watatakiwa kutumia Biblia zao. Hakikisha kwamba wote wamejibu swali hilo vizuri.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 16:12-15. Wale wengine wasikilize yale ambayo Yesu alisema Roho Mtakatifu angewafanyia wafuasi wake. Sasa waambie wajibu swali la pili. Rudieni pamoja majibu hayo.

Sema: Roho Mtakatifu alifanya kazi katika maisha ya wanafunzi wa Yesu, naye yuko tayari kufanya kazi maishani mwetu ikiwa tutamkubalia. Jibuni swali hili, Je, unamtegemea Roho Mtakatifu kama Msaidizi na Mwalimu? (Waeleze jinsi watakavyotakiwa kuchora mviringo kando ya usemi ambao unaeleza wakati wanapopaswa kumtegemea Roho Mtakatifu awasaidie na kuwafundisha.)

1. Naye akiisha kuja, huyo ATAUHAKIKISHIA ulimwengu kwa habari ya DHAMBI, na HAKI, na HUKUMU.

2. Roho Mtakatifu atawafanyiaje wale waliompokea Yesu Kristo kama Mwokozi? (Yohana 16:12-15).
3. Huyo Roho wa kweli ATA-WAONGOZA awatie kwenye KWELI yote. Atawapasha habari ya MAMBO YAJAYO.

Je, unamtegemea Roho Mtakatifu kama Mwalimu na Msaidizi? Chora mviringo kando ya usemi ufuatao ambao unaeleza wakati unapopaswa kumtegemea Roho Mtakatifu kukufundisha na kukusaidia.

-unapokata tamaa

-unapojawa na woga

-unapokuwa na matatizo ya kijamii

-unapofikiria kuwa wenzako hawa-kupendi.

-unapokuwa mgonjwa

Umuruhusuje Roho Mtakatifu kuwa Mwalimu na Msaidizi?

Tafuta katika Biblia yako Wagalatia 5:22-23. Haya ni maandiko yaelezayo mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Andika majina tisa ya tunda la Roho katika picha ya mti ufuatao.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Lakini yeye atakapokuja, huyu Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote"
(Yohana 16:13).


Thomas alikuwa mchoyo sana. Kila mara aliwalaani wenzake na akafurahia sana kufanya hivyo. Aligombana na watoto wengine. Aliwatendea wanyama ukatili. Hakuwa na rafiki ye yote na

alisema kwamba hata hakuwahitaji. Hatimaye alikubali Yesu kama Mwokozi wake na akajazwa na Roho Mtakatifu. Rafiki zake walianza kuona kuwa amebadilika sana. Aliacha kulaani na akanza kufikiria mahitaji ya watu wengine. Hangeweza kujitea mabadiliko haya. Uwezo wa Roho Mtakatifu ndio uliobadili maisha ya Thomas.

Roho Mtakatifu ni msaidizi mkuu.

WAKATI WA MWISHO

Waongoze wanafunzi hao katika kukariri kifungu cha kukumbuka. Tumia mfano ulioko katika kifungu cha kukumbuka kuonyesha jinsi Roho Mtakatifu alivyo Msaidizi mkuu. Hakikisha kwamba watoto wanaelewa jinsi Roho Mtakatifu awezavyo kuwasaidia. Funga kwa kumwomba kila mmoja aweze kufahamu kuwepo kwa Roho Mtakatifu maishani mwake.



SURA YA KUMI NA MOJA

MUNGU WA REHEMA

MASOMO YA BIBLIA: Waefeso 2:1-10

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Masomo ya miezi hii mitatu yamekuwezesha kuwaeleza wanafunzi wako mpango wa wokovu. Je, kuna wavulana na wasichana ambao wamemkubali Kristo kama Bwana na Mwokozi wao? Je, wametambua kwamba hawakufanya lo lote ili wapate wokovu?

Pengine baadhi ya wanafunzi watafikiria kwamba Mungu amewaokoa kwa kuacha kutenda maovu au kwa sababu wanawatendea wenzao mema. Somo hili litakuwezesha kuwaelezea vyema kwamba mtu huokolewa kwa sababu ya neema za Mungu tu.

Mara kwa mara watu hufikiria kwamba ni lazima wampendeze Mungu ndipo awape kile watakacho na kuwabariki. Ujumbe wa Biblia ni kinyume cha wazo hili. Kwa kweli, mtu anapaswa kuamini. Ni lazima atubu dhambi zake na aamini kwamba Mungu atamsamehe. Lakini hawezi kutenda tu wema ili apate wokovu. Hii ni karama ya Mungu. Mungu ni mwenye kurehemu.

Jihoji jinsi uelewavyo. Je, unaelewa maana ya rehema za Mungu? Ndiyo, unajua kwamba neema ni upendo na rehema, ambavyo hukustahili kupata. Lakini je, unaelewa jinsi rehema ilivyobadili maisha yako? Mruhusu Roho wa Mungu kunena nawe na

kukusaidia mahitaji yako unapojitayarisha kufundisha somo hili.

Somo hili ni la muhimu sana. Kwa hivyo, unapaswa kujiandaa vilivyo ili uweze kuwaongoza wanafunzi wako kuona maana yake maishani mwao.

Utahitaji ubao au karatasi kubwa ya kufundishia somo hili. Njoo na kalamu pia, za kuwapa wanafunzi wako.

Sura ya kwanza na ya pili ya Waefeso inaeleza kuhusu mpango wa wokovu wa Mungu katika Yesu Kristo. Soma sura hizi zote ili uelewe zaidi.

Wakati wa kufundisha utatumia Waefeso 2:1-10. Vifungu vya kwanza vitatu vinaeleza tabia za asiyemwamini na kile cha 4 hadi 7, vyote vinaeleza yale Mungu awafanyiayo waamini.

Paulo, katika kifungu cha 1 hadi 3 anasema kwamba yule asiye na Kristo amekufa kiroho. Mtu kama huyu hana uzima wa kiroho. Hata hawezi kufanya lo lote la kumpendeza Mungu. Yeye amekufa kiroho kwa sababu ya "makosa na dhambi zake." Neno hili "makosa" hutumiwa kwa kuelezea mtu aliyepotea njia. "Dhambi" nayo ni "kukosa shabaha." Kufanya dhambi ni kukosa kuwa jinsi Mungu alivyo-tuumba.

Mtu asiye na Kristo huwa si mtiifu. Hajali Neno la Mungu. Huwa anaongozwa na mambo ya ulimwengu. Humruhusu shetani amwongoze ili amwasi Mungu.

Yule asiyemwamini hutawaliwa na dhambi. Hufanya jinsi atakavyo.

Hawezi kuokolewa kwa sababu ya matendo yake. Huwa amehukumiwa kifo kwa sababu hana Mungu.

Kifungu cha 4 hadi 7, vinatueleza yale ambayo Mungu huwafanyia waamini. Mungu alitupenda tulipokuwa wenye dhambi. Mungu ni pendo. Asili yake hasa ni kupenda. Wakati awaonyeshapo wenye dhambi upendo huu huwa sasa ndiyo neema na rehema. Mwanadamu hawezi kujiokoa mwenyewe, lakini sisi huweza kupata wokovu kwa ajili ya neema na rehema za Mungu. Mungu hutupa kile ambacho hutustahili kupata kwa sababu ni mwenye huruma.

Mungu alitufufua tulipokuwa wafu katika dhambi. Agano Jipya linatuambia aina tatu za mifano jinsi Yesu alivyowafufua wafu. Ufufuo huu wa kweli unaonyesha picha ya ufufuo wa kiroho ambao mwenye dhambi hupata apokeapo karama ya wokovu wa Mungu katika Kristo. Ufufuo huu wa kiroho hutufanya tuwe na ushirika na Kristo. Huwa tumepata uzima wa kiroho.

Mungu hutuina na kutujaza kiroho ili tuwe pamoja naye sasa na hata milele. Mkristo anaweza kuwa anaishi kimwili hapa duniani, lakini sasa anafurahia ushirika wake na Mungu katika Yesu Kristo. Naye afapo kimwili, ataenda kuishi na Baba yake huko mbinguni, milele na milele.

Kusudi la somo hili ni *kulinganisha mtu aliyepotelea dhambini na yule aliye na uzima katika Kristo ili wanafunzi waweze kuelewa kwamba wanaweza kuokolewa tu kwa neema ya Mungu.*

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je, mnapenda kupokea barua? Sema: Mlipokea barua moja wiki hii. Hebu tuisome tena. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome barua hii iliyoko mwanzoni mwa somo hili.)

Sema: Barua hii ni mfano wa Paulo asemavyo na wewe sasa. Hebu sasa tusome jinsi alivyowaandikia watu wa kanisa la Efeso.

Soma maandiko ya Biblia. Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waefeso 2:1-3, na mwingine asome Waefeso 2:4-7. Eleza kwamba vifungu vya kwanza vitatu vinatoa maelezo ya yule asiyemwamini na kwanzia 4 hadi 7, vinaeleza yale Mungu amfanyiayo mwamini.

Waulize wanafunzi kutaja tabia za asiye mwamini huku ukiandika majibu yao katika upande wa kushoto wa ubao au kwenye karatasi kubwa.

Asiye mwamini huwa:

1. amekufa kiroho.
2. hamtii Mungu wala kujali Neno lake.
3. anaongozwa na shetani katika kumwasi Mungu.
4. hufanya jinsi atakavyo (hutawaliwa na dhambi).

Waulize sasa wanafunzi kusema yale ambayo Mungu huwafanyia waamini. Andika majibu yao ubaoni, upande wa kulia.

Yale Mungu huwafanya waamini:

1. Humpenda wakati angalipo mwenye dhambi na humwokoa kwa neema yake.

2. Humfanya awe na uhusiano wa haki wa Kristo.
3. Humpa uzima (uhai).
4. Humwinua kiroho ili awe pamoja naye sasa na hata milele.

Mpe kila mwanafunzi kalamu na umwambie aandike ile orodha ya kwanza ielezayo habari za mtu asiye mwamini. Orodha hii inapaswa kuandikwa juu ya jiwe la kaburi lililoko katika somo lao. Pengine baadhi yao walikuwa wameandika orodha hii waliposoma somo hili.

Waulize baadhi yao kusoma jambo waliloandika ambayo hufanyika wakati mtu afufuliwapo pamoja na Kristo. Waambie waandike chini ya sentensi hiyo mambo matatu ambayo yanatuambia vile Mungu awafanyavyo waamini.

Uliza: Je, kifungu cha sita kinatoa ahadi gani?

Sema: Hatujui jinsi mbinguni kulivyo. Lakini Biblia inatuambia ni mahali pa ajabu. Chora umbo unalofikiria utakuwa nalo kule mbinguni. (Wanafunzi nao watapaswa kuchora picha zao katika nafasi iliyoachwa yenye kichwa hiki, "Makao ya mbinguni.")

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waefeso 2:8-10.

Uliza: Neno "neema" lina maana gani? (Ngojea majibu.)

Sema: "Neema" ni upendo na rehema ambazo hutustahili kupata. Tunastahili kufa kwa dhambi zetu, lakini Mungu alimtuma Yesu aje kutufia. Neema ya Mungu imetuwezesha kupata uzima wa

kiroho. Ametuokoa kutoka mautini. Hatuwezi kufanya cho chote cha kulipia wala kupewa wokovu huu. Wokovu ni karama ya Mungu. Sisi tunapaswa tu kuamini na kuupokea wokovu huu.

Waongoze wanafunzi hao kusema kifungu cha kukumbuka ambacho ni Waefeso 2:8.

Mwambie mmoja wao asome tena kifungu cha 10, mwingine asome aya ya mwisho ya barua iliyoko katika vitabu vyao.

Sema: Matendo mazuri hayawezi kutuokoa, lakini baada ya Mungu kutuokoa hututaka tumfanyie kazi. Angalieni somo letu chini ya kichwa kisemacho "Eneza Habari ya Kristo Ulimwenguni." Je, Mungu anakutaka ufanyeje ili ueneze upendo wa Kristo ulimwenguni? Orodhesha mambo hayo.

KAZI YA KUFANYA

Sehemu hii itakusaidia kuongoza wanafunzi wako katika kuelewa maana ya somo hili maishani mwao.

Hakuna majibu yaliyotolewa katika sehemu ya kwanza. Kila mwanafunzi anapaswa kujibu jinsi afikiriavyo maisha ya mtu asiye na Kristo huwa. Wanafunzi watajibu sehemu hii vizuri wakijifunza kuandika majibu hayo kwa maneno yao wenyewe.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Waefeso 2:8).

Waongoze wanafunzi hao kukariri kifungu cha kukumbuka ikiwa hawakijui. Eleza maana ya neno "neema" ikiwa kunaye mwanafunzi ambaye halielewi.

WAKATI WA MWISHO

Angalia tena kundi lako la kufundisha. Je, wanafunzi hao wameelewa mabadiliko yatokeayo maishani mwa mtu awapo Mkristo? Je, wameelewa mwenye kuleta mabadiliko haya?

Unapaswa kusesitiza kwamba wokovu ni kipawa cha Mungu, ikiwa kunao wale ambao hawajamwamini Kristo. Mungu alitupenda sana hata akamtoa mwanawe badala yetu. Mungu ni mwenye rehema na anaweza kumwokoia mtu ye yote ambaye ana imani ya kumwamini.

Kwa wale ambao ni Wakristo waweza kuwahimiza kwa kusema kwamba tumeokolewa kwa ajili ya kusudi fulani. Wakristo ni wafuasi wa Kristo. Wao ni wafanya kazi wake hapa ulimwenguni.

Funga kwa maombi ya kumwomba kila mmoja akue katika neema ya Mungu.

YESU ALIKUFA KWA AJILI YETU

MASOMO YA BIBLIA: Marko 15:22-39; Warumi 3:20-26

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wakati kama huu kila mwaka Wakristo huwa wanakumbuka hasa kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo. Umesikia mara nyingi sana hadithi ya kusulubiwa kwa Yesu msalabani. Unajua vyema jinsi ilivyokuwa. Lakini, ni rahisi kukosa kuelewa maana ya kifo cha Kristo. Utatakiwa kufikiria kuhusu ushirika wako na Mungu unaposoma Maandiko ya somo hili. Maisha yako yalikuaje kabla ya kumpokea Kristo? Je, kwa sasa kuna mabadiliko gani? Je, maisha yako yangukaje ikiwa Kristo hangekufia?

Baadhi ya vijana katika darasa lako wanafahamu sana hadithi ya kusulubiwa kwa Yesu. Lakini, pengine wengi wao hawajawahi kufikiria sana kuhusu kifo cha Yesu. Unapaswa kuwasaidia ili waelewe jambo ambalo Yesu alifanya alipokufa msalabani. Halafu pia uwasaidie kuelewa kwamba alifia kila mmoja wao. Mwongoze kila mtoto katika kufikiria mabadiliko ambayo kifo cha Kristo chaweza kuleta maishani mwake.

Usitumie muda wako mwingi ukieleza habari za kusulubiwa. Lakini uwe na muda wa kutosha wa kueleza Warumi 3:20-26. Ni habari ngumu sana kueleza na unaweza kushawishika ili uisome tu bila kueleza. Unapaswa kusoma kwa uangalifu ili uelewe ujumbe huo. Wazo lililoandikwa hapa chini laweza kukusaidia.

Kila mojawapo wa Injili inaeleza habari za kufa kwa Yesu Msalabani. Kiini ni kile, lakini kila mwandishi anaeleza kwa mtindo wake. Unaweza kusoma pia vifungu vifuatavyo: Mathayo 27:27-54; Luka 23:26-49 na Yohana 19:17-30.

Katika Marko 15:31-32 tunaona jinsi viongozi wa Kiyahudi walivyo mdhihaki Yesu. Walimwambia mara nyingi ajishushe kutoka msalabani. Yesu alikuwa na uwezo wa kujitoa msalabani, lakini hakutaka kufanya hivyo. Alijua kwamba kifo chake ndicho kingemwezesha mwanadamu kuwa na ushirika na Mungu. Yesu alikuja kuwaambia watu habari za upendo wa Mungu. Zaidi ya hapo, yeye mwenyewe alikuwa upendo wa Mungu. Ikiwa angeshuka toka msalabani, angekuwa akisema kwamba, "Upendo wa Mungu una mwisho." Lakini Yesu alikuwa tayari kuteseka na kufa kwa ajili ya mwanadamu. Tunajua kwamba upendo wa Mungu hauna mwisho kwa sababu ya kifo cha Yesu. Ujumbe wa msalaba ni kwamba upendo wa Mungu hauna kipimo. Ni upendo utakao-kuwepo hadi mwisho.

Je, tunaelewa maana ya Yesu kuchukua dhambi za ulimwengu wote? Soma kifungu cha 33 hadi 39. Sasa soma tena kifungu cha 34. Hatuwezi kuelewa yote yaliyotendeka. Yesu alikuwa ameteseka sana. Biblia inatuambia kwamba alikuwa ameshapitia majaribu yote ambayo humpata mwanadamu. Lakini, kwa sababu Yesu hakuwa ametenda

dhambi, alijitwika dhambi za kila mmoja. Muda huu ulimfanya afahamu maana ya kutengana na Mungu kwa ajili ya dhambi. Hatuwezi kufahamu jinsi Yesu alivyojisikia wakati huu. Alikuwa kila mara mkamilifu mbele za Mungu. Hakuwa amejua jinsi ilivyo kutengana na Mungu. Hata hivyo, Yesu alimpenda mwanadamu sana hata akawa tayari kuteseka kwa ajili yake.

Soma Warumi 3:20-26. Paulo alikuwa akijibu swali aliloulizwa wakati huo na ambalo watu wangali wanaliuliza. Je, mwenye dhambi anawezaje kuwa na ushirika mwema na Mungu.

Katika kifungu cha 20 na 21, tunaambiwa kwamba kutii sheria hakuwezi kutupa haki ya Mungu. Na hakuna mtu ye yote ambaye amewahi kutii sheria zote. Sheria humwonyesha mtu dhambi aliyo nayo. Kifungu cha 23 kinatambia kwamba sote tumefanya dhambi. Je, hatuwezi kuwa na ushirika na Mungu? Je dhambi itakuwa tu ikitutenganisha naye?

Jibu ni "la". Kifo cha Yesu msalabani kilimfanya mwanadamu kuurudia ushirika wake na Mungu.

Katika kifungu cha 24 na 25, tunaambiwa mambo matatu muhimu ambayo Yesu alifanya alipokufa msalabani.

Kwanza, **ALIMKOMBOA** mwanadamu. Kila mtu ni mtumwa wa dhambi. Na ni Yesu tu awezaye kumfanya huru. Kulikuwapo na wakati ambapo watu waliuzwa sokoni kama watumwa. Wengine waliuzwa na kununuliwa mara nyingi. Kama bwana mkubwa alikuwa amemwaza mtumwa wake na

akaamua kumununua tena na kumwachilia huru, ilimbidi amnunue kwa bei ghali. Sasa bwana mkubwa alikuwa amemkomboa mtumwa huyo. Hivi ndivyo Yesu alivyomkomboa mwanadamu. Mwanadamu alikuwa mtumwa wa dhambi, naye alipaswa kufa. Lakini alinunuliwa tena kwa kifo cha Yesu na kuwa huru.

Pili, Paulo anasema kwamba kifo cha Yesu kilimletea mwanadamu **HAKI**. Yesu alikuja kutuambia kwamba, Mungu angali anatupenda hata ingawa tu waovu. Hatupaswi kumkimbia jinsi watoto wasio watiifu wakimbiavyo wazazi wao. Yesu alipokufa msalabani alitupa haki ya kumwendea Mungu. Yeye hutuondolea hatia tulionayo. Sisi tunapaswa tu kuamini kwamba ametutimizia haya yote.

Kifungu cha 25 kinasema kwamba Mungu alimtoa Yesu "awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake." Hii inamaanisha kwamba Yesu alitoa sadaka ya dhambi zetu. Wayahudi walikuwa wakitoa dhabihu ya mnyama walipotenda dhambi. Walifanya hivi ili waweze kutakaswa na kusamehewa. Mungu hakuhitaji tena dhabihu hiyo. Yesu alikuwa "mwana-kondoo" aliyetolewa dhabihu ya dhambi za mwanadamu. Hakupaswi kuwepo dhabihu nyingine ye yote.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi kuelewa sababu ya Yesu kufa msalabani na kuwaongoza ili waitikie upendo huu mkuu.

KULIFUNDISHA SOMO

Unaweza kuanza somo hili kwa kusimulia hadithi ya Samweli iliyoko katika kitabu cha wanafunzi iwapo

hawajasoma somo hili kabla ya kuja darasani. Iwapo wamelisoma, utapaswa kuwauliza maswali yahasuyo tukio hilo. Linganisha hadithi hiyo na jinsi Yesu alivyotoa maisha yake ili awaokoe wanadamu waliopaswa kufa.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Marko 15:22-39. Au pengine unaweza kuwasomea vifungu hivyo. Kabla ya kusoma waambie wanafunzi hao wajifikirie kuwa walikuwepo wakati wa kusulibiwa kwa Yesu. Baada ya kuwasomea vifungu, wape muda wa kujadili maswali yafuatayo: Je, unafikiri kuwa Yesu alijitoka kufa msalabani au alifanya hivyo kwa sababu hangeweza kuamua jambo la kufanya? (Waambie kwamba alikuwa na uwezo wa kujitoka msalabani iwapo angetaka hivyo.) Unadhani ni kwa nini aliwaacha askari hao wamsulubishe? (Alitaka kutimiza lile lililomleta ulimwenguni, yaani, kumwokoa mwanadamu kutoka dhambini.)

Jadilianeni maana ya kifungu cha 34. (Tazama maelezo yake katika sehemu juu.)

Waambie wanafunzi fulani wasome Warumi 3:20-26. Kila mmoja anaweza kusoma vifungu viwili au vitatu.

Uliza: Kulingana na kifungu cha 20, je, tunaweza kuwa na amani na Mungu kwa kutii sheria? (Kutii sheria hakuwezi kumfanya mtu awe mwenye haki. Hakuna ye yote ambaye ameweza kutii sheria zote. Sheria humwonyesha mtu dhambi aliyonayo.)

Uliza: Kwa nini hatuna amani na Mungu? Ni nini kilicholeta utengano baina yetu na Mungu? (Dhambi)

Chora picha kubwa ubaoni au kwenye karatasi kubwa katika upande wa kushoto ionyeshayo jinsi dhambi ilivyotutenganisha na Mungu. Sasa chora nyingine tena upande wa kulia ionyeshe jinsi Yesu alivyokufa msalabani na kutupatanisha na Mungu.




Tumia maelezo yaliyo katika kitabu cha wanafunzi na yale yaliyoko katika sehemu ya "Kujiandaa Kufundisha" ya kitabu chako kueleza maana ya maneno haya komboa, haki, na dhambi. Andika kila neno ubaoni na ulieleze. Tumia lugha rahisi.

KAZI YA KUFANYA


Huu ndio wakati wa kujua jinsi wanafunzi walivyoelewa. Jambo muhimu ni kwamba unapaswa kuwasaidia ili waelewe maana ya somo hili maishani mwao.

Hakuna majibu yaliyotolewa kwa sehemu ya kwanza ya KAZI YA KUFANYA kwa sababu kila mwanafunzi atatakiwa kujibu jinsi alivyoelewa. Waonyeshe jinsi ya kujibu na uwahimiza wajibu. Pengine utataka kuzungumzia baadhi ya majibu hayo.

Yesu alifanywa dhambi ya dhambi zetu aliposulubiwa msalabani. Hatuwezi tena kutoa dhambi ya kondoo ili tusamehewe dhambi zetu. Yesu ndiye mwana kondoo aliyejitwika



dhambi za ulimwengu wote. Yafikirie yote uliyojifunza katika somo hili na ujibu maswali yafuatayo:



Kwa nini Yesu alijitoa kufa msalabani? _____

Je, jambo hili linaonyesha kuwa anakujali pamoja na mahitaji yako? _____

Je, utaitikiaje upendo huu wa Mungu? _____

Fungua tena katika somo lako mahali walipoelezea Warumi 3:20-26.

Utapata maneno matatu yaliyo andikwa katika herufi kubwa yanayosema yale aliyokufanyia Yesu alipokufa msalabani. Maneno yenyewe yameandikwa hapo chini lakini hayasomeki vizuri. Yapange vizuri na uyaandike katika nafasi iliyoachwa.

Je, Yesu alipokufa msalabani alinifanyaje?

1. ALINIKOMBOA. (AKALIMBOANI)
2. Alinihesabia HAKI. (KIHA)
3. Alitolewa kama DHABIHU ya dhambi zangu. (DHAHIBU)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8).

Fanya mazoezi ya kusema kifungu hiki pamoja na watoto. Unaweza kufanya mashindano. Ligawe darasa katika makundi mawili. Mwambie kila mmoja aandike kifungu hicho. Sasa anza kuhesabu ili uone kikundi kilicho na wengi walioandika vyema kifungu hicho.

WAKATI WA MWISHO

Wahimiza watoto ili wafikirie jinsi Mungu anavyowapenda. Waweza kuwahimiza pia wale ambao hawajakata shauri la kumfuata Kristo kufanya hivyo. Waongoze wale walio Wakristo kuufikiria upendo wao kwa Yesu na jinsi wawezavyo kuonyesha wenzao upendo huo.

Funga kwa maombi.

SURA YA KUMI NA TATU

KRISTO AMEFUFUKA

MASOMO YA BIBLIA: 1 Wakorintho 15:12-28

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Pengine vijana wa darasa lako wamesikia mengi kuhusu kuishi tena baada ya kufa. Hii haimaanishi kwamba wanaelewa yale yasemwayo katika Agano Jipya kuhusu jambo hili. Baadhi ya wanafunzi wamewasikia jamaa wasio Wakristo wakiongea habari za kifo. Wanaweza kuchanganyikiwa na yale mambo ya kimila waliyoyasikia. Wengi wameona baadhi ya jamaa yao wakifa. Hushangaa kwa kile kilichowapata wapendwa wao. Somo hili litakuwezesha kuwasaidia wanafunzi wako kuelewa yale Biblia isemayo kuhusu kufufuka. Kuelewa huku kutawapa tumaini na kuwaondolea woga wa mauti. Kutawafariji wale hawajui la kufikiria kuhusu kufufuka.

Wiki hii utatakiwa kufundisha kifungu cha kukumbuka kwa mtindo tofauti. Andika kila neno kwa kijikaratasi na uwe tayari kuwapa wanafunzi unapofundisha somo hili.

Utatakiwa kusoma kwa makini 1 Wakorintho 15. Hata hivyo, utataka kujua maana halisi ya vifungu hivyo. Soma sura hiyo yote. Unaposoma, kumbuka mambo haya mawili. Kwanza, sura ya 15 inaeleza habari za kufufuka katika wafu. Paulo alihubiri kuhusu ufufuo. Aliamini kwamba mtu alikombolewa na Mungu alipomkubali kwa imani. Naye alipewa uzima wa sasa na hata baada ya kufa. Mungu aliwafufua walio wake katika wafu.

Ilikuwa vigumu kwa Wagiriki kuamini fundisho hili la ufufuo. Wao waliamini kwamba roho iliendelea kuishi, lakini hawakuelewa jinsi mtu awezavyo kuwa na mwili wa kiroho baada ya kufa. Hata baadhi ya Wakristo wa Korintho walikuwa na tatizo hili. Paulo, katika sura hii yote, amejaribu kuwaelezea jinsi mwili huo utakavyokuwa baada ya kufufuliwa.

Jambo la pili ambalo litakusaidia kuelewa sura hii ni hili. Hasa Paulo anaongea kuhusu ufufuo wa waamini akiulinganisha na ule wa Kristo.

Soma tena 1 Wakorintho 15:12-19. Kifungu cha 12 kinadhihirisha sababu iliyomfanya Paulo awaandikie Wakristo hao wengi kuhusu ufufuo. Hakuna dhihirisho lionyeshalo kwamba waliukataa ufufuo wa Kristo. Lakini baadhi yao hawakuamini kwamba wao wangepufuliwa. Paulo alisema kwamba ufufuo wa waamini wa Kristo ni kitu kimoja. Alisema kwamba ingekuwa ni upumbavu kukubali ufufuo wa Kristo na kutokubali ufufuo wa waamini.

Pengine Paulo aliguswa sana kiroho alipoandika vifungu vya 12 hadi 19. Alizungumzia hasa jambo lile lile tu katika vifungu hivi. Yaliyo ya muhimu katika sehemu hii ni haya:

1. Ikiwa wafu hawafufuki, basi Kristo naye hakufufuka (kifungu cha 13 na 16).
2. Kuhubiri wala imani haina maana ikiwa Kristo hajafufuka na

waamini wangali wanaishi katika dhambi (kifungu cha 14 na 17).

3. Wahubiri wa Injili ni mashahidi wa uongo iwapo hakuna ufufuo haupo (kifungu cha 19).
5. Watu watabakia tu wafu iwapo Kristo hajafufuliwa (kifungu cha 18).



Soma 1 Wakorintho 15:20-28. Vifungu hivi vinatuambia ushindi ulioko katika ufufuo wa Kristo na ule wetu.

Kifungu cha 20 kinaanza na maneno haya, “Lakini sasa.” Hii ilikuwa njia ya Paulo ya kusema kwamba hata ikiwa wengine hawataamini kuwa Kristo hakufufuka, yeye ameishafufuka katika wafu naye ni limbuko la waliolala.

Neno “limbuko” limetolewa hasa katika Agano la Kale. Katika Mambo ya Walawi 23:10, neno hili limetumiwa kuonyesha mganda wa mavuno ya kwanza yaliyotolewa kwa Mungu kama sadaka. Limbuko hili lilikuwa ishara ya mavuno yajayo.

Vivyo hivyo Kristo hakuwa tu wa kwanza kufufuka, bali alikuwa ishara

ionyeshayo mavuno yajayo. “Mavuno” haya ni kufufuliwa kwa waamini.

Paulo, katika kifungu cha 21 na 22 amesema kwamba mauti yaliletwa na Adamu alipokataa kumtii Mungu. Lakini, kutii kwa Kristo na kufa kwake msalabani kulileta uzima. Wale wanaomtii na kumwamini Kristo wataishi.

Paulo anaendelea kuandika habari za mpango wa ufufuo katika kifungu cha 23 na 24. Maana iliyoko hapa ni kwamba Kristo atarudi kabla ya waamini kufufuliwa. Kuja kwake kutadhihirisha kuwa “mwisho” umewadia.

Katika kifungu cha 25 hadi 28 tunapata maelezo ya kile kitakachofanyika wakati wa kurudi kwa Yesu. Lakini jambo la muhimu ni kwamba Mungu baba atatawala katika Ufalme wake kwa sababu Mwanawe amemtayarishia Ufalme ambao ameshinda kila adui wake. Adui wa mwisho atakayeshindwa ni mauti.

Sehemu inayobakia ya sura hii haitajadiliwa sasa. Paulo ametumia sura kwa kueleza kwa ukamilifu habari za mauti na ufufuo mpaka imejulikana kama “Sura ya Ufufuo.” Sura hii inawawezesha waamini wote kujua kwamba mauti sio mwisho, bali ni mwanzo mpya.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi kufahamu ukweli wa Biblia kuhusu ufufuo na kuwawezesha kuyaendea mauti bila woga bali na tumaini.*

KULIFUNDISHA SOMO

Anza somo kwa kuimba wimbo uhusuo ufufuo. Chagua wimbo ambao kila mwanafunzi anaujua.

Waulize wanafunzi waseme nyimbo ambazo wanajua zihusuzo ufufuo.

Sema: Nyimbo hizi zote zinahusu ufufuo. Lakini kuna jambo ambalo hufanyika kabla ya kufufuka, nalo ni mauti.

Wāambie wanafunzi hao waseme jinsi walivyoshuhudia kifo cha jamaa zao au rafiki zao. Wahimize wasimulie kilichofanyika na jinsi walivyojisikia. Vijana wengi wameshuhudia vifo, lakini baadhi yao hayajawahi kusimulia habari yake. Uwe tayari kutoa mfano ikiwa wanafunzi hao wataogopa kusimulia.

Vijana hawawezi kuepuka palipo na kifo. Kwa hivyo, huu ndio wakati mzuri wa kutoa maoni yao.

Sema: Somo la leo litakusaidia kuelewa yale Biblia isemayo kuhusu kufufuliwa kwa Wakristo.

Sema: Huwa hatupendi sana kuongea habari za kifo, hali tunayo maswali mengi ya kujiuliza. Baadhi ya majibu ya maswali haya yanaweza kupatikana katika “Kujiandaa Kufundisha.” Wakorintho wa kwanza 15 inasema mengi kuhusu kifo na kufufuliwa.

Waambie wanafunzi sababu iliyomfanya Paulo kuandika sura hii.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome 1 Wakorintho 15:12-19 na uwaambie wale wengine kusikiliza yaliyo muhimu kwa Wakristo, ambayo

hayangekuwa na maana iwapo Kristo hangefufuka katika wafu. Yaandike ubaoni na uwaambie wanafunzi hao wayaandike katika sehemu yao ya kwanza ya KAZI YA KUFANYA. (Utapata orodha ya mambo haya katika nafasi iliyoachwa ya KAZI YA KUFANYA.)

Wasomee 1 Wakorintho 15:20-28. Waambie wayafuate kwa makini maandiko haya wakisikiliza mambo yawafurahishayo wasikiapo kuwa Kristo amefufuka. Andika majibu yao ubaoni. Majibu yao yanapaswa kulingana na mambo yaliyoko katika sehemu ya pili ya KAZI YA KUFANYA.

Wape muda wa kujaza nafasi zilizoachwa katika sehemu ya pili.

Tumia maelezo yaliyoko katika sehemu ya “Kujiandaa Kufundisha” kueleza maana ya maneno kama “limbuko”, “katika Adamu wote wamekufa”, na “katika Kristo wote watahuishwa.”

Uliza: Je, kulingana na kifungu cha 23 na 24 Yesu atakuja lini? Eleza kwamba Biblia haituambii wakati Yesu atakapokuja. Haitoi utaratibu wote, bali inatuhakikishia kwamba Yesu atarudi tena.

Wasomee 1 Wakorintho 15:57. Sisitiza ushindi tulionao kutokana na kifo na kufufuka kwa Kristo. Ikiwa kunao wale ambao wanaogopa kifo, wahakikishie kwamba ushindi wa Kristo utakuwa pia ushindi wa wale walio watoto wake, yaani waamini.

KAZI YA KUFANYA

Bwana Kamau aliongoza kundi la wanafunzi katika kutafuta maana ya 1 Wakorintho 15:12-28. Aliwaambia watafute kuanzia kifungu cha 12 hadi 19, yale yaliyo muhimu kwa Wakristo ambayo hayangekuwa na maana iwapo Kristo hangefufuliwa katika wafu. Taja mambo haya kwa kukamilisha sentensi zifuatazo.

1. KUHUBIRI kungekuwa bure tu. (kifungu cha 14)
2. IMANI yenu ingekuwa bure. (kifungu cha 14)
3. Tungekuwa MASHAHIDI wa uongo wa Mungu. (kifungu cha 15)
4. Tungekuwa tungali katika DHAMBI zetu. (kifungu cha 15)
5. Hakungekuwa na tumaini la waamini WALIO KUFA katika Kristo. (kifungu cha 18)

Sasa soma kuanzia kifungu cha 20 hadi 28. Ni mambo gani uliyopata ambayo yanakufurahisha usikiapo kuwa Kristo amefufuka katika wafu? Soma vifungu hivi na ukamilishe sentensi zifuatazo.

1. Wale waliokufa hawatabaki wakiwa WAFU. (kifungu cha 20 hadi 22)
2. Wale ambao watakuwa bado HAI wakati Kristo atakapokuja, lakini wao ni mali yake, watakuwa na uhakika kwamba watakuwa na ushindi wa Kristo juu ya MAUTI. (kifungu cha 23)
3. Maadui wote watashindwa katika Kristo...hata adui wa mwisho ambaye ni MAUTI. (kifungu cha 24 hadi 26)

4. Mwishowe MUNGU atakuwa mtawala wa vitu vyote. (kifungu cha 28)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye" (Warumi 6:8).

Mwanzoni mwa wiki hii uliandika maneno ya kifungu hiki kwenye vijikaratasi tofauti tofauti. Mpe kila mwanafunzi kijikaratasi kilicho na neno moja. Ikiwa wanafunzi hao hawazidi kumi na tatu, utapaswa kumpa kila mmoja zaidi ya kijikaratasi kimoja.

Waambie sasa wayasome maneno hayo jinsi, yanavyofuatana katika kifungu. Wa mwisho kusoma atakuwa yule mwenye kumbukumbu yake. Waambie waangalie katika Biblia au kwenye KIFUNGU CHA KUKUMBUKA iwapo wanahitaji msaada.

Rudia zoezi hili hadi wanafunzi hao watakaposoma maneno haya jinsi yalivyo. Sasa waambie wakariri kifungu hicho pamoja. Wakoseapo neno moja, mwambie mwanafunzi aliye nalo kuwajulisha. Rudieni kifungu hicho hadi watakapoweza kukisema bila kusaidiwa.

WAKATI WA MWISHO

Sema: Unapaswa kuelewa ukweli wa kifungu cha kukumbuka iwapo unataka kukabili kifo na tumaini na bila woga. Wale wanaompokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wao wataishi naye milele kwa sababu yeye yu hai.

Ikiwa kunao ambao hawajampokea Kristo hakikisha kwamba wameclewa vizuri jinsi ya kufanya hivyo.